# Nipashe

Jumamosi Aprili 24, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580560

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11

**Gwajima** alia na sheria uhujumu na utakatishaji

UKURASA 3



**Nape** ataka tume huru kuchunguza maslahi ya walimu

UKURASA 3



# Askofu achambua hotuba ya Samia

UKURASA 2

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**RAIS SAMIA, MTENDAJI MKUU SADC WATETA**

RAIS Samia Suluhu Hassan, jana alikutana na kuzungumza na Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya...

UKURASA WA 4

**MBUNGE ADAI KUTISHIWA MAISHA NA MKUU WILAYA**

MBUNGE wa Songwe (CCM), Philipo Mulugo, amemtuhumu Mkuu wa Wilaya....

UKURASA WA 8

**MAKANDARASI WAZALENDO WAIANGUKIA SERIKALI**

MAKANDARASI wazalendo wameiangukia serikali wakiomba wapewe zabuni nyingi za ujenzi...


## Wahofiwa kufa kwa kusombwa na maji

UKURASA 2




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), Dk. Agnes Kijazi, akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, kuhusu mwenendo wa kimbunga 'Jobo' kwenye pwani ya Tanzania. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Tahadhari yatolewa kimbunga Jobo

UKURASA 2





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play

Download on the App Store



**MICHEZO** MOSHI MWEUPE SIMBA SC NA FCC UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Wahofiwa kufa kusombwa maji

**Na Mary Mosha, HAI**

WATU watatu wanahofiwa kufa maji katika Kata ya Masama Mashariki, Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, baada ya kudaiwa kusombwa na mafuriko ya maji ya Mto Namwi juzi baada ya kunyesha mvua kubwa.

Jana, Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, alithibitisha watu hao mpaka sasa hawajulikani waliko na wanahofiwa kufa maji kutokana na gari lao walilokuwa wamepanda kusombwa na maji na kuharibiwa vibaya.

"Hivi sasa kuna jitihada zinafanyika kuwatafuta watu hao, ambapo kikosi maalum kinachohusisha waokoaji na jeshi la akiba na wananchi wanawatafuta usiku na mchana.

"Kuna madaraja zaidi ya sita yameng'olewa na maji hayo, hivyo tunaenda kukaa kuona namna ya kuyarudisha kwa udharura wake," alisema.

Ole Sabaya alisema walipata taarifa za tukio hilo majira ya saa tisa usiku na walianza kuwasaka watu hao saa 11 alfajiri na walifanikiwa kuona mabaki ya lori hilo.

"Tuko kwenye msako tangu saa 11 alfajiri. Tulipata taarifa majira ya saa tisa usiku. Kikosi maalum kinachohusisha askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi (JWTZ) kinaendelea kuwatafuta," alisema. Kiongozi huyo wa wilaya alisema eneo hilo lilikuwa halijapata mvua kubwa kwa kiwango hicho katika miaka 50 iliyopita, akibainisha kuwa tayari ameshawasiliana na ngazi za juu kufanya tathmini ya madhara ya mvua hiyo.

Mbunge wa Hai (CCM), Saashisha Mafuwe, ametuma salamu za pole kutokana na maafa hayo, akieleza kwamba tayari amekwiwasiliana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kitengo cha Maafa kwa ajili ya kuwasaidia wananchi hao na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, kwa ajili ya hatua zaidi.

Wanaohofiwa kufa maji ni dereva Godson Ngowi na wasaidizi wake wawili, Elia Lema na Godfrey Uroki.

Inadaiwa kuwa watu hao walikwenda kupakia ndizi vijiji vya jirani lakini ilipofika saa tano usiku, mmiliki wa gari hilo, Cuthbert Uroki aliwatafuta kwa simu ili kupata taarifa, lakini hawakupatikana.

"Niliendelea na jitihada hizo hadi alifajiri na nilipoamka kwenda Soko la Mulla, nilipofika daraja la Mto Namwi nilipata taarifa ya gari langu kusombwa na maji, "alisema

Diwani wa Machame Mashariki, Martin Munisi, alisema maji hayo yameharibu mali za watu pamoja na gari lililokuwa limebeba ndizi kutoka kwa wakulima kwenda katika Soko la Mulla.

Pia, inadaiwa kuwa kata zaidi ya nne zimeathirika na mafuriko hayo ikiwamo Machame Mashariki, Weruweru, Masama Mashariki na Masama Uroki.



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Dk. Stergomena Lawrence Tax, Ikulu ya Chamwino, mkoani Dodoma jana. Habari Uk. wa 4**. PICHA: IKULU**

# Bagonza aichambua hotuba ya Samia

**Na Beatrice Moses**

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Karagwe, Dk. Benson Bangoza, ameichambua hotuba ya Rais, Samia Suluhu Hassan, aliyoiwasilisha bungeni juzi, akimpongeza kiongozi huyo wa nchi kwa kugusa haki za binadamu.

Mbali na haki za binadamu, Askofu Bagonza amempongeza Rais Samia kwa kuweka wazi nia yake ya kuimarisha demokrasia na ustawi wa vyama vya siasa.

Katika andiko lake kuhusu hotuba hiyo, lililosambazwa kwenye mitandao ya kijamii jana, Askofu Bangoza alibainisha kuwa hotuba ya Rais Samia ni nzuri.

"Yaliyo mengi tumeyashika tangu utoto. Yalienda likizo awamu ya tano, kawa jasiri kugusa demokrasia na haki za binadamu. Vigelegele vilipungua. Sababu ipo. Awamu iliyopita haikuwa rafiki wa demokrasia na haki za binadamu... Ninampongeza hata kwa kusema, kutenda tunasubiri," alisema.

Katika andiko lake hilo, Askofu Bagonza pia aligusia suala la sheria, akitahadharisha kuwa huenda kukawa na mgongano kwa kuwa Rais Samia kwenye hotuba yake anavitaka vyombo vya haki vitoe haki kwa mujibu wa sheria, lakini baadhi ya sheria zilizopitishwa hivi karibuni ni mbaya.

"Haki ipi mbele ya sheria mbaya? Sheria mbaya huzaa haki mbaya. Kaahidi kukutana na vyama vya siasa, bila shaka alimaanisha vya upinzani kwa sababu cha kwake si cha siasa ni cha dola. Ahadi inasubiriwa. ahadi imekosa vigelegele, walipita bila kupingwa na demokrasia ikafa bila kupingwa," alisema.

"Mwisho wa mwezi, Mama (Samia) anakalia kiti cha chama dola chetu, baada ya hapo akutane na vyama vya siasa, akiwa nao atasahau kuwa yeye ni Mwenyekiti wa chama dola?" alihoji.

Askofu Bangoza pia alimpongeza Rais Samia kwa kuruhusu serikali yake kukosolewa, akisema "tumuombee".

Alisema hotuba imegusa vitu vingi na anamshukuru Rais Samia, huku akibainisha kuwapo vitu alivyotamani vizungumzwe na Rais Samia katika hotuba hiyo, lakini havikujumuishwa.

Kutokana na hali hiyo, Askofu Bagonza alisema atatafuta nafasi ya kuzungumza na Rais Samia.

"Nilitamani Katiba Mpya aliyoiongoza, maridhiano na wahanga wa awamu iliyopita, matamko yaliyokiuka katiba na yanaendelea kutekelezwa, nina mengine, nitamtafuta mama. Ninamwombea mama, ameshikilia mustakabali wetu, kazi iendelee," alisema.

# Tahadhari yatolewa kimbunga Jobo

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa (TMA), imeendelea kuwataka wananchi katika mikoa ya Lindi, Mtwara na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Mafia na Zanzibar kuchukua tahadhari kutokana na uwapo wa kimbunga Jobo kinachotarajiwa kufika mwambao wa pwani ya Tanzania kesho.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Agnes Kijazi, alisema kuwa mpaka kufikia leo mchana, kimbunga hicho kinatarajiwa kuwa umbali wa Km 125 mashariki mwa Kisiwa cha Mafia na kesho usiku kinatarajiwa kufika pwani ya Dar es Salaam.

"Ingawa kimbunga hiki kinazidi kupungua nguvu kadri kinavyokuja, bado tahadhari lazima zichukuliwe kwa sababu tunatarajii mpaka kufika Dar es Salaam, kitakuwa na nguvu ya spidi ya Km 60 kwa saa. Kwa nguvu hii bado kinaweza kuleta madhara, hivyo lazima tahadhari zichukuliwe," alisema Dk. Kijazi.

Alisema kutakuwa na upepo mkali unaokadiriwa kuwa na spidi hiyo ya Km 50 mpaka 60 kwa saa.

"Wananchi wanatakiwa kuendelea kufuatilia taarifa zinazotolewa na mamlaka na pia kufuata maelekezo na miongozo inayotolewa na wataalamu wa sekta husika ili kupunguza athari zinazoweza kutokea," alisema.

Akizungumzia historia ya kimbunga hicho kilichoanzia kaskazini mwa Kisiwa cha Madagascar, Dk. Kijazi alisema si kawaida kutokea kwa vimbunga nchini.

"Nchi yetu ipo karibu sana na Ikweta, mara nyingi vimbunga hivi vinatokea kusini zaidi ya Ikweta, hiki kinachotarajiwa kufika hapa kwetu, kwa mara ya mwisho kilitokea Dar es Salaam mwaka 1872.

"Pia kiliwahi kutokea Lindi mwaka 1952, hivyo ukiangalia ni nadra sana kutokea kimbunga hapa kwetu," alisema Dk. Kijazi, akibainisha kuwa kimbunga Jobo kikifika Dar es Salaam, hakitachukua muda mrefu kupotea baada ya kufika nchi kavu.

"Vimbunga vingi vinatokea baharini lakini vikija nchi kavu havichukui muda mrefu vinapotea, pamoja na kuwa tunakitegemea kimbunga Jobo kufika huku kwetu, hali inaweza kubadilika na kubadili mwelekeo kama ilivyokuwa kwa kimbunga Kenedy ambacho kiliishia pwani ya kusini mwa Afrika huko Msumbiji ingawa kilionekana kuja huku kwetu," alifafanua.

Alisema athari zinazotarajiwa, zitatokea maeneo ya Kanda ya Ziwa kutokana na mkandamizo wa hewa ambapo unatarajiwa kuvuta unyevunyevu kufika misitu ya Congo na kusababisha mvua kwa baadhi ya maeneo ya Tanzania.

# Gwajima alia na sheria za uhujumu, utakatishaji

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

MBUNGE wa Kawe, Josephat Gwajima (CCM), ameliomba Bunge na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, kuziangalia upya sheria tatu alizoziita kandamizi, zilizojaa uonevu na kusababisha Watanzania wengi kuswekwa mahabusu.

Alizitaja sheria hizo kuwa; Sheria ya Utakatishaji Fedha, Sheria ya Uhujumu Uchumi na Sheria ya Ugaidi.

Akichangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, bungeni jana, Gwajima alisema kuna Watanzania wengi wako mahabusu kwa sababu ya kubambikwa makosa ya utakatishaji fedha na watu wasio waaminifu.

"Bunge hili wakati linapitisha sheria hizi na kufikia mahali kwamba hakuna dhamana kabisa. Nia ya Bunge ilikuwa ni nzuri lakini utekelezaji wake umeingia dosari kubwa.

"Kuna watu wengi wapo mahabusu kwa sababu ya kubambikiziwa kosa la utakatishaji fedha na watu wasio waaminifu. Kwa nchi makini, hili suala haliwezi kuacwa hivi hivi, unakuta mtu anakwenda kwa mfanyanyabiashara kudai mapato au malimbikizo ya mapato, anakwenda na hati ya mashtaka kwamba asipopewa kiasi fulani cha fedha anampa kesi ya uhujumu uchumi au utakatishaji fedha," alisema.

Gwajima alisema kwa takwimu alizopata hadi sasa, kuna watu 1,701 waliopo mahabusu kwa sababu ya ama utakatishaji fedha au uhujumu uchumi.

"Kwa kuwa kazi mojawapo ya Bunge ni kutunga sheria na kufuta sheria, haileti maana wale masheikh wa uamsho 23 wa Zanzibar wapo mahabusu hadi leo. Leo ni miaka tisa.

"Ninajaribu kuwaza ningekuwa mimi au baba yangu yupo mahabusu kwa miaka tisa pasipo kuhukumiwa halafu baada ya miaka 20 mkagundua hana hatia, mtawalipa nini?

"Lakini haitoshi, kuna masheikh 64 huko mkoani Arusha ambao wako mahabusu kwa sababu ya Sheria ya Ugaidi ambayo haina dhamana. Mimi sielewi kwanini masheikh tu ndiyo magaidi? Kwani hakuna watu wengine ambao ni magaidi?

"Waziri husika tafuta namna ya kushughulia sheria hizi, siyo haki masheikh hawa kuwa mahabusu kwa miaka tisa, sisemi kama wana hatia au hawana, hoja yangu ni kuwa mahabusu kwa kipindi hicho pasipo kuhukumiwa, ni vyema wakahukumiwa ili wajue wamebakiza miaka mingapi," alishauri.

Katika kuweka mkazo wa hoja yake, Gwajima alisema kuna rafiki yake alifuatwa na watu wakamwambia ama atoe Sh. milioni 100 au wampe kesi ya utakatishaji fedha.

## MCT yaanzisha kanzidata masahibu ya wanahabari

**Na Christina Haule,** MOROGORO

BARAZA la Habari Tanzania (MCT), limeanzisha kanzidata ya madhira yanayowapata wanahabari yatakayosaidia kuongeza nguvu ya ushahidi wakati wa kesi mbalimbali za kuzuia Uhuru wa wanahabari.

Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mukajanga, alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya uhuru wa habari na haki ya kupata taarifa kwa waandishi wa habari kutoka mikoa mbalimbali yaliyoandaliwa na baraza hilo yanayofanyika mjini hapa.

Alisema kuna wanahabari wamekuwa wakipigwa na kunyimwa uhuru wao wa kupata taarifa na pengine kuvunjiwa vifaa vyao vya kazi jambo ambalo si sahihi kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016.

Ukusanyaji kanzidata hiyo, alisema utasaidia kuongeza ushawishi na utetezi kwa wanahabari wanapokumbwa na madhira na kwamba ikiwa itasema sheria ina upungufu mbalimbali, inabidi kuwe na ushahidi.

Mukajanga alisema kupatikana kwa data zinazohusiana na upatikanaji wa taarifa kutaleta njia rahisi ya haki ya kupata taarifa kwa wanahabari wakati wanapofanya ushawishi na uzengezi.

Naye Mratibu kutoka MCT, Saumu Mwalimu, aliitaka jamii kutambua kuwa kila mtu anahaki ya kupata taarifa na kwamba wapo wananchi wengi bado hawajajua hilo.




Askari Polisi wa Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU) Mkoa wa Iringa, wakiimarisha ulinzi, wakati madereva Bajaji walipoandamana wakishinikiza mwenzao kuachiwa baada ya kukamatwa katika mgomo walioufanya, mjini Iringa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Nape Nnauye ataka tume kero za walimu

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

MBUNGE wa Mtama, Nape Nnauye (CCM), ameitaka serikali kuunda tume maalum ya kuchunguza matatizo ya walimu, akisisitiza wameathiriwa na mifumo, kunyimwa stahiki zao ikiwamo kutopandishwa madaraja, mishahara, kupunjwa mafao pamoja na stahiki zinginezo zinazowahusu.

Amesema walimu nchini wamekuwa wakinyimwa haki na stahiki zao na kutothaminiwa, kunakosababishwa na wizara na Hazina kutoa nyaraka na taratibu ambazo zimekuwa haziwatendei haki.

Nape aliyasema hayo bungeni jana alipochangia majadala wa makadirio na matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Hazina pamoja na baadhi ya wizara wamekuwa wakitoa nyaraka na taratibu ambazo zimekuwa haziwatendi haki walimu.

Mbunge huyo aliyewahi kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, alisema nyaraka hizo na taratibu zimezaa makundi mbalimbali kwa walimu.

Nape alilitaja kundi la kwanza la walimu waliokumbana na baa hilo kuwa ni la waliopewa barua za kupandishwa madaraja, lakini stahiki zao hazikubadilika hadi walipostaafu, na kusababisha mafao yao kuathirika kwa kiwango kikubwa.

Alitaja kundi la pili ni walimu waliopandishwa madaraja kwa barua, lakini hakukuwa na mabadiliko katika stahiki zao kwa muda mrefu, hadi wakakutwa na barua zingine za kupandishwa madaraja wakati zile za kwanza hazikufanyiwa kazi, akisisitiza kundi hilo wako wengi.

Nape alitaja kundi la tatu liliothiriwa ni walimu ambao walipandishwa madaraja au vyeo kwa karatasi, lakini mpaka leo wamebaki na maandishi ya pesa kwenye karatasi bila mabadiliko kwenye stahiki zao.

Alitaja kundi la nne ni walimu waliopandishwa madaraja kwa barua tangu mwaka 2013, wakakaa na barua hizo bila ya mabadiliko ya stahiki zao na baada ya muda, ukaandikwa waraka kufuta upandishaji wao wa madaraka pasipo sababu za msingi.

Kutokana na hali hiyo, Nape alisema: "Serikali iunde tume maalum ikachunguze suala hilo ili wale ambao tayari wameshaathiriwa na huu mfumo, tuwarekebishie mambo yao hata ikiwezekana tuwalipe taratibu, lakini haki yao isipotee."

Alisema Chama Cha Mapinduzi (CCM) ni chama cha wakulima na wafanyakazi, hivyo serikali ya CCM ni muhimu ikashughulika na wafanyakazi kama mtaji.

Alisema asilimia 70 ya watumishi wa umma nchini ni walimu na ndiyo kundi lililokabidhiwa watoto ili liwalee na kuwafundisha kutengeneza taifa la leo na la baadaye.

"Mimi ninadhani serikali walifuta waraka wa walimu waliopandishwa madaraja kwa sababu walitaka kukwepa malimbikizo ya madeni, ndiyo maana wakaandika waraka wa kufuta. "Haya madaraja na stahiki zao siyo hisani, ni haki zao. Hivi linavyoendeshwa, inaonekana kama ni hisani wakati siyo kweli, ni haki yao," Nape alionya.

Alisema hatua ya serikali kuweka mkakati wa kuwapandisha madaraja walimu 90,000 ni mzuri, lakini isiwasahau wa zamani. Nape alisema nyaraka zinazoandikwa kutoka Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora pamoja na Hazina zisiwe kichaka cha kupora haki za walimu.

Akijibu hoja hiyo wakati wa kuhitimisha majadala huo, Waziri wenye dhamana ya Utumishi, Mohamed Mchengerwa, alisema watapitia nyaraka zote zilizotolewa kwa walimu. Waziri huyo alisema endapo kutabainika kuwapo zilizotolewa pasipo kufuata sheria, zitafutwa. Hata hivyo, alisisitiza kuwa tangu aingie ofisini, hajakutana na waraka uliokiuka utaratibu.

HABARI KITAIFA

## Sheria ya uwekezaji kufanyiwa mabadiliko

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Geoffrey Mwambe, amesema serikali imechukua hatua kubadilisha sera na sheria mbalimbali ambazo zinasimamia uwekezaji na biashara ili kuhakikisha wawekezaji mazingira mazuri ya biashara.

Waziri Mwambe aliyasema hayo jana wakati wa kikao cha pamoja kilichoandaliwa na Shirikisho la Wenye Viwanda (CTI) na Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) na kuwakutanisha wafanyabiashara.

Alisema iko Sheria ya Biashara ya mwaka 2003 ambayo ni ya siku nyingi inayofanyiwa mabadiliko hivi sasa.

"Mapitio yanafanyika kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara. Pia ipo Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997, imeshafanyika mchakato wa kwanza kupitia sera yake tangu mwaka 2013. Mpaka mwaka 2016 mchakato wa kuanzisha sheria mpya ulikuwa umeshaanza. Kwa sasa ipo kwenye hatua za mapitio ya mwisho, kabla ya kupekekwa kwenye kamati ya wataalam na baadaye kwenye baraza la mawaziri na baadaye bungeni," alisema.

Waziri Mwambe alisema wiki ijayo watafanya kikao cha kupitia sheria ya uwekezaji mpya kwa hiyo kutakuwa na mawazo mengi mapya yameingizwa na mtazamo wa sekta binafsi na wa Rais Samia Suluhu Hassan namna ya kuboresha utendaji na kuipa nguvu Kituo cha Uwekezaji (TIC).

"Tumejipanga kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara na CTI ni mfano watumie fursa zilizopo kufanya biashara zao, ili kufanya hivyo nimewaambia wawajibike, moja, wengi wamekuwa wakidanganya serikali hasa kwenye ulipaji wa kodi.

"Wanatumia mbinu tunaiita wanabana faida isionekane kwa kuweka gharama nyingi kwa mizania ya faida na hasara ambayo ni mapato na matumizi," alisema akisisitiza kuwa linafanyika na unakuta kampuni ni ya muda mrefu lakini inaonyesha haijapata faida.

Kuhusu marejesho ya kodi ambayo hubakiwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Waziri Mwambe alisema wengi wamekuwa wakidanganya na baadhi walipeleka namna au risiti za uongo na matokeo yanaonyesha wanadai serikali fedha nyingi kuliko uhalisia. "Baada ya ukaguzi tangu mwaka 2016 ilionekana kuna baadhi wanaodai siyo wakweli, hivyo serikali iliamua kuwakagua wote tena kwa kutumia uwakiki kwa husisha aliyetoa hiyo huduma kwa anayedai," alisema.

Alisema serikali imeshafanya uhakiki na madeni yamedhibitika ni sahihi yanalipwa kupitia fedha zinazotengwa kila mwezi.



Msajili wa Bodi ya Makandarasi nchini (CRB), Rhoben Nkori (katikati), akijadiliana jambo na Mwenyekiti wa bodi hiyo, Consolatha Ngimbwa (kushoto) na Makamu Menyekiti wa bodi hiyo, Joseph Tango, kabla ya kuanza kwa mkutano wa makandarasi 300, jijini Mbeya juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mbunge adai kutishiwa maisha na DC

**Na Thobias Mwanakatwe, SONGWE**

MBUNGE wa Songwe (CCM), Philipo Mulugo, amemtuhumu Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Samuel Jeremiah, kwamba ametishia kumuua.

Amedai kuwa chanzo cha kutishiwa na mkuu huyo wa wilaya ni kutokana na kumfuatilia kuhusu matumizi ya fedha za michango ya wawekezaji na anadai kwamba anamkwamisha kufanya maendeleo wilayani hapa.

Mulugo alimweleza hayo Jumatano wiki hii, Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia jenerali Nicodemus Mwangela, mbele ya kikao cha wadau wa zao la ufuta kilichojumuisha watendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe, madiwani, wanunuzi wa zao hilo, viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na wakulima.

Hili ni tishio la pili la kutishia kuuawa kwa kiongozi baada lile la Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Mbozi, Hanji Godigodi ambaye alidai kutishiwa kuuawa na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Songwe, Henerico Mkola, na taarifa za tukio hilo kuripotiwa kituo cha polisi Vwawa na namba (RB) MBZ/IR/200/2021.

Akizungumza katika kikao hicho, Mulugo alisema vitisho dhidi yake kutoka kwa mkuu huyo wa wilaya, vimekuja baada ya kuwa mstari wa mbele kuwatetea wakulima wa zao hilo ambao hawako tayari kwa sasa kupeleka mazao yao kuuza kwa mfumo wa stakabadhi ghalani uliokuwa umetangazwa na serikali ya wilaya.

Mbunge huyo alisema mkuu huyo wa wilaya pia haelewani na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya, jambo ambalo amesema si jema kwenye uongozi na linakwamisha maendeleo.

Naye Katibu wa CCM wa Wilaya ya Songwe, Gerald Mwadalu, alipopewa dakika mbili kuzungumza, alimwambia mkuu wa mkoa kuwa kiongozi huyo wa wilaya hana uhusiano mzuri pia na madiwani na viongozi wa chama.

Mwadalu licha ya kukatishwa mara kwa mara na Mkuu wa Mkoa wakati akizungumza, alidai kuwa chama kimejitahidi mara kadhaa kumwita kwenye vikao ili wajadiliane lakini mara zote amekuwa akikaidi.

Katibu huyo alimkabidhi Mkuu wa Mkoa nyaraka kuhusu mwenendo wa mkuu huyo wa wilaya.

Wakati katibu huyo akiendelea kuzungumza huku akirekodiwa na waandishi wa habari, ghafla mkuu wa mkoa aliingilia kati na kuamuru waandishi wa habari kuacha kurekodi mambo anayoyasema.

Pia Mwengela aliagiza polisi kuzishikilia kamera za waandishi hao kabla ya kutoka katika ukumbi wa halmashauri hiyo ambako mkutano huo ulikuwa ukifanyika.

Akijibu tuhuma hizo, Jeremiah alisema kwa kifupi kuwa kama mbunge huyo anao ushahidi wa jambo hilo la kutishiwa maisha, anapaswa kwenda kutoa taarifa polisi.

Naye Mwengela aliingilia kati na baadaye akasema mbali na kuwapatanisha viongozi hao huko nyuma na kudhani yameisha, amejionea hali halisi ilivyo na kwamba kwa hekima alizojaliwa atazidi kuketi nao kwa ajili ya kuleta mshikamano.

# Samia, mtendaji mkuu SADC wateta

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, jana alikutana na kuzungumza na Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Dk. Stergomena Tax, ambaye alimpa taarifa juu ya masuala mbalimbali yahusuyo jumuiya hiyo.

Katika mazungumzo hayo yaliyofanyika Ikulu, Chamwimo mkoani Dodoma, yalihudhuriwa pia na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula.

Taarifa iliyotolewa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu jana, ilisema katika mazungumzo hayo, Dk. Tax alimpongeza Rais Samia kwa kushika madaraka ya urais na kuwa Rais wa Kwanza mwanamke Tanzania.

Pia taarifa hiyo ilisema Dk. Tax alimpongeza Rais Samia kwa hotuba nzuri aliyoitoa Bungeni juzi ambayo imetoa mwelekeo wa serikali ya awamu ya sita.

Dk. Tax ambaye anamaliza muda wake wa miaka minane Agosti, mwaka huu, aliishukuru Tanzania kwa ushirikiano alioupata wakati wote akiwa Katibu Mtendaji wa SADC na kuipongeza wakati wa uenyekiti wake wa SADC, kuandaa na kukamilisha mkakati wa maendeleo wa jumuiya licha ya kuwapo kwa changamoto za janga la corona duniani.

Pia alisema katika nafasi hiyo, Tanzania imekifanya Kiswahili kuwa lugha rasmi ya SADC, kuanza mradi wa uwekaji sanamu ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere katika Umoja wa Afrika (AU) na uendelezaji wa gesi.

Dk. Tax pia alisema katika kipindi hicho, SADC imeendelea kuwa na utulivu wa kisiasa ambao umetoa fursa nyingi za maendeleo ya kiuchumi, hivyo kutoa wito kwa Tanzania kutilia mkazo katika uimarishaji wa sekta za uzalishaji kama vile viwanda, kilimo, biashara, kusimamia ubora na kuendeleza miundombinu.

Kwa upande wake, Rais Samia alimpongeza Dk. Tax kwa kuiwakilisha vizuri Tanzania katika utumishi wake akiwa Katibu Mtendaji wa SADC na ameahidi kufanyia kazi ushauri na fursa mbalimbali ambazo SADC inazitoa kwa Tanzania.

Rais Samia pia alimkaribisha nyumbani Dk. Tax baada ya kumaliza muda wake ili aungane na Watanzania katika ujenzi wa taifa.

TANGAZO

# LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA
Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037, E-mail: lhrc@humanrights.or.tz
Website www.humanrights.or.tz

## Barua ya Wazi kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Haki ya Kuishi kama ilivyobainishwa kweny Ripoti ya Haki za Binadamu (LHRC), 2021

**Waheshimiwa Wabunge,**
Salaam za dhati ziwafikie, hongereni kwa kuendelea na kazi ya kuijenga Taifa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwakilishi wenu bungeni kwa niaba ya wananchi katika Bunge la 12.
Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kinaandika barua hii wazi kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutambua mamlaka yake ya kikatiba ya kufanya maamuzi ya msingi kwa maslahi mapana ya Taifa. Kwa mwaka 2020, LHRC ilifanya utafiti kuhusu hali ya haki za binadamu ikiwa na dhima iitwayo, tisho la virusi vya korona dhidi ya uimarishaji na ulindaji wa haki za binadamu, katika mikoa yote ya Tanzania na kutoa mapendekezo ya kisera ili kuboresha mazingira ya utekelezaji wa haki hizo kwa mwaka 2021.

**Haki ya Kuishi**

**Waheshimiwa Wabunge,**
Haki ya kuishi ni haki iliyo kwenye kundi la haki za kiraia na kisiasa, andiko hili limeangazia haki ya kuishi kwa kuangalia hali ya mwaka 2019 na 2020 nchini kama ilivyoelezwa katika Ripoti ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, 2020, kwa kuangalia sababu nane (8) zilizohatarisha ustawi wa haki hii; matukio ya kujichukulia sheria mikononi; mauaji yanayofanywa na vyombo vya dola; matukio ya ukatili dhidi ya vyombo vya dola; matukio ya mauaji yanayotokana na imani za kishirikina; adhabu ya kifo; matukio ya ajali za barabarani na mauaji yanayotokana na wivu wa kimapenzi.

Ni muhimu kwanza kufahamu mikataba ya kimataifa na sheria zinazotambua na kulinda haki hii, kuna mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa, 1966; Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu, 2006; Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto, 1989; Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto, 1990; Mkataba wa Maputo unaolinda haki za wanawake, 2003; Mkataba wa Jumuiya ya nchi za Kusini mwa Afrika unahusu Jinsia na Maendeleo, 2008. Pia, Tamko la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu la mwaka 1948.

Kwa Tanzania, haki ya kuishi inatambulika katika ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhri ya Muungano wa Tanzania,1977.

**Sababu zinazopelekea kuvunjwa kwa haki ya kuishi**

**i. Matukio ya kujichukulia sheria mkononi**

Katika kipindi cha miaka mitano (2015-2019) matukio ya vitendo vya watu kujichukulia sheria mikononi ambapo matukio zaidi ya 3200 yaliripotiwa kutoka katika takwimu za Jeshi la Polisi nchini. Hii ni sawa na wastani wa mauaji 640 kwa kila mwaka au matukio 53 kila mwezi, ambapo matukio hayo yalitokea maeneo ya vijijini na miji midogo. Kwa mwaka 2020, Jeshi la Polisi limeripoti matukio 443 ya mauaji ambapo tathimini inaonesha matukio yamepungua kwa idadi ya matukio 254 ikilinganishwa na mwaka 2019.

**ii. Mauaji yanayofanywa na vyombo vya dola, matukio ya ukatili dhidi ya vyombo vya dola**

Ni ukweli kwamba, vyombo vya dola vinajukumu la kulinda usalama kama ilivyoanishwa katika Kanuni za Maadili ya Maafisa wa Utekelezaji wa Sheria iliyopitishwa na Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa kwa azimio namba 34/169 ya tarehe 17 mwezi wa 12 mwaka 1979.

Katika kipindi cha mwaka 2020 LHRC ilirekodi jumla ya matukio manne (4) ya mauaji yaliyofanywa na vyombo vya dola yaliyotokea mkoa wa Tabora, katika wilaya ya Kaliua ambapo tukio hili lilifanywa na askari mgambo dhidi Juma Rajabu (40) kwa kushindwa kulipa shilingi 1,000 kwa ajili ya ujenzi wa choo cha shule ya Msingi Ushokola. Tukio lingine liliripotiwa kutoka mkoa wa Mbeya ambapo maafisa wa TANAPA walimuua ndugu Ulandi Dotto (28), mkazi wa Kijiji cha Mwavala katika wilaya ya Mbarali kwa kuingiza mifugo yao katika mbuga ya Ruaha. Katika mkoa wa Dar es salaam matukio mawili (2) yaliripotiwa; mnamo tarehe 21/02/2020 Bwana Walker Muhame alipigwa hadi kufa akiwa chini ya uangalizi wa polisi; tarehe 21/01/2020 tukio la nne katika mkoa wa Dar es salaam litokea katika kata ya Manzese, wilaya ya Ubungo kwa Bwana Salum Sefu (30) kupigwa askari mgambo kwa amri ya Mwenyekiti wa mtaa na kusababisha kifo chake.

Mwaka 2019 LHRC ilirekodi matukio matatu (3) ikilinganisha na mwaka 2020 kuwa na matukio manne (1). Hali hii inaonesha kuongeza kwa tukio moja zaidi la mauaji yalifanywa na vyombo vya dola.

**iii. Matukio ya mauaji yanayotokana na imani za kishirikina**

Takwimu zinaonesha kupungua kwa matukio ya mauaji kwa imani za kishirikina kutoka matukio 189 mwaka 2019 hadi matukio 112 mwaka 2020 yaliyorekodiwa na Jeshi la Polisi. Matukio hayo hufanywa na wanajamii kwa imani potofu za kishirikina, Tanzania ni miongoni mwa nchi yenye kasi kubwa ya matukio haya. Kwa kipindi cha miaka mitano kutoka mwaka 2015 hadi 2019 zaidi ya matukio 1,380 sawa na wastani wa matukio 276 kwa mwaka au matukio 23 kila mwezi.

LHRC ilikusanya matukio 13 ya mauaji yaliyoripotiwa kutoka mkoa wa Geita, Rukwa, Katavi, Tanga, Mbeya, Njombe na Kigoma.

Waheshimiwa wabunge, andiko hili linaleta takwimu hizi kwenu, ili kuchukua hatua na jitihada madhubuti kwa ajili ya kuishauri Serikali ili kuweka mipango ya kumaliza kabisa matukio hayo. Matukio haya yanaashiria kwamba, bado kuna uelewa mdogo wa wananchi kuhusu namna za kitaalamu za kutatua matatizo.

**iv. Adhabu ya kifo**

Mnamo mwezi Mei 2016, Umoja wa Mataifa ulitoa mapendekezo kwa Tanzania ya kufuta adhabu ya kifo katika mchakato wa mapitio hali ya haki za binadamu (Universal Periodic Review), msingi wa mapendekezo ya Umoja wa Mataifa ulizingatia ukweli wa kwamba, adhabu ya kifo inapingana na haki ya kuishi.

Kwa mwaka 2020 ripoti ya LHRC ya haki za binadamu ili rekodi jumla ya kesi 30 za hukumu ya adhabu ya kifo katika kipindi mwezi Januari hadi Desemba. Kituo kilifarijika sana na nia ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Joseph Magufuli kwa kutoa adhabu mbadala kwa wafungwa 256 waliyohukumiwa kunyongwa, kwa kuwabadilishia na kuwapa adhabu ya kifungo cha maisha.

Mara ya mwisho Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutekeleza adhabu ya kifo ilikuwa mwaka 1994 chini ya uongozi wa Rais wa awamu ya pili, Mh. Ali Hassani Mwinyi. Pamoja na kutokutekelezwa kwa adhabu hiyo toka mwaka 1994, bado Mahakama za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinatoa adhabu ya kifo kwa mtu atakayetiwa hatiani kwa kosa la mauaji. Mahakama kuwa na uwezo wa kutoa adhabu hiyo, utekelezaji wake unategemea saini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano ambaye ataridhia utekelezaji wa adhabu hiyo kwa mtu kunyongwa.

**v. Ajali za barabarani**

Waheshimwa wabunge, LHRC imechambua Takwimu za matukio ya ajali za barabarani zilizotolewa na Jeshi la Polisi, katika eneo hili serikali imefanya jitihada kubwa za kupunguza matukio ya ajali za barabarani mwaka 2016 yaliripotiwa matukio 10,297; mwaka 2019 yaliropotiwa matukio 2,924 sawa na kusema kwamba matukio ya ajali za barabarani yalipungua kwa asilimia 56%. Kwa upande mwingine, mwaka 2016 iliripotiwa vifo 3,381 vilivyo sababishwa na ajali za barabarani hadi kufikia mwaka 2019 vifo 1,536 sawa na kupungua kwa asilimia 38% ya vifo vilivyosababishwa na ajali za barabarani.

Katika kipindi cha kuanzia mwezi wa Januari hadi Julai 2020 jumla ya vifo 229 viliripotiwa na Jeshi la Polisi kutokana na ajali za barabarani ikilinganishwa na vifo 247 kwa kipindi cha mwezi Januari hadi Juni 2019.

Pia, vifo vitokanavyo na ajali za pikipiki viliripotiwa kupungua kutoka 157 katika kipindi cha mwezi Januari hadi Juni 2019 kufikia vifo 124 kutoka mwezi Januari hadi Juni 2020. Kwa wastani jumla ya watu 2,621 waliripoti kufa kwa ajali za barabarani katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2019.

Waheshimwa wabunge, pamoja na jitihada kubwa zilizofanywa na serikali kuzibiti ajali za barabarani bado juhudi zaidi inahitajika ili kupunguza zaidi na hatimae kumaliza ajali za mara kwa mara ili kulinda haki ya kuishi ya watu wasiyo na hatia.

**vi. Wivu wa kimapenzi**

Eneo hili bado linachangamoto inayohitaji ufumbuzi wa haraka, wanawake wamekuwa wahanga wa kubwa na vipigo na vitendo vya ukatili vilivyosababisha kupotea uhai. LHRC kwa mwaka 2019 ilirekodi jumla ya vifo 12 vya wanawake waliyouawa na wenza wao. Kwa mwaka 2020, jumla ya vifo 32 vya wanawake rekodiwa na LHRC, hii ni kiashiria kwamba kuna tatizo kubwa katika jamii linalohitaji msaada wa haraka wa kimifumo na rasilimali ili kudhibiti kabisa ukatili huu.

**Mapendekezo yetu**

1. Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuendeleza juhudi za kusimamia mipango ya serikali dhidi ya matukio ya kujichukulia sheria mkononi hususani kwa kuweka kipaumbele kwenye bajeti ili kuongeza elimu kwa jamii kuhusu madhara ya kujichukulia sheria mikononi.

2. Wabunge kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha kwamba hakuna chombo cha dola au mtu yeyote atakayejichukulia sheria mkononi.

3. Wabunge kufanya kazi kwa ukaribu na viongozi wa dini ili kuelimisha na kukemea vitendo vitokanavyo na imani za kishirikina.

4. Kuishauri serikali kutotekeleza na kuifuta adhabu ya kifo, kwa kuwa inatweza utu wa haki za binadamu. Pia,ni wakati muafaka kwa Tanzania kuungana na Jumuiya ya Kimataifa, pamoja na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika (mathalani nchi ya Rwanda, Msumbiji, Burundi, Togo, Congo, Gabon, Benin, Guinea, Bukinafaso na Madagascar) kufuta adhabu hii kwenye vitabu vya sheria.

5. Serikali kuendeleza juhudi za kuboresha mifumo ya kuripoti matukio ya vitendo hatarishi barabarani pamoja na usimamizi madhubuti wa mifumo hiyo. Pia, kufanya marekebisho ya maeneo hatarishi yanayoweza kusababisha ajali za barabarani.

6. Bunge kufanya tathmini ya Mpango wa Kupinga Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (NPA-VAWC) unaoisha mwaka huu 2021, na kutunga mpango mpya utakao wekewa bajeti ili kutokomeza vitendo vya kikatili vinavyosababisha vifo vya wanawake katika jamii.

**Hitimisho**

LHRC inaimani kubwa kwamba, waheshimiwa wabunge mnanguvu na mamlaka ya kufanya marekebisho, kusimamia na kupitisha sera, sheria pamoja na mipango madhubuti ya kulinda haki ya kuishi nchini. Haki ya kuishi ndiyo msingi mkuu wa haki zote, hivyo inapaswa kulindwa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Makocha Yanga lengo liwe kujenga timu na si ubingwa

HATIMAYE uongozi wa Klabu ya Yanga umetangaza benchi jipya la ufundi litakaloongozwa na Kocha Mkuu, Mtunisia Nasreddine Nabi, ambaye ametua na wasaidizi wake wawili, akichukua rasmi mikoba ya Mrundi Cedric Kaze aliyetimuliwa Machi 7, mwaka huu, kutokana na mwenedo mbaya wa matokeo ya timu hiyo.

Nabi anakuwa kocha wa tatu kwa Yanga msimu huu kwani awali mabingwa hao wa kihistoria wa Ligi Kuu Bara, walianza msimu na Mserbia Zlatko Krmpotic, ambaye naye alitimuliwa na kurithiwa na Cedric.

Kwa ujumla kutimuliwa kwa makocha hao wawili, Zlatko na Kaze kulitokana na uongozi kupata msukumo ['presha'] mkubwa kutoka kwa mashabiki ambao wamekuwa wakitoa sababu kadha wa kadha ama hawaridhiki na kiwango cha timu hiyo au matokeo, lengo kubwa likiwa ni ubingwa msimu huu.

Kitu ambacho wamekuwa wakikitaka mashabiki na wanachama wa Yanga na kutoa presha kubwa kwa uongozi wa klabu hiyo, ni kuona timu yao kwanza ikicheza soka la kuvutia lakini pia ikipata matokeo yatakayoiwezesha mwisho wa msimu kutwaa ubingwa.

Hakuna ubishi kwamba katika timu ya mpira wa miguu popote duniani, pamoja na mambo mengine yote ikiwamo kutengeneza faida, lakini lengo kubwa na furaha ya mashabiki ni kuona timu yao ikibeba mataji, malengo mengine husalia kwa viongozi.

Lakini katika hilo kwa Yanga, mashabiki, wanachama na hata viongozi hawana budi kutambua kwamba huu ni msimu wa pili mfululizo, timu hiyo inafanya usajili mkubwa kuanzia dirisha kubwa hadi dogo kwa kubadilisha idadi kubwa ya wachezaji jambo ambalo huwa linahitaji muda ili timu kupata muunganiko mzuri.

Na kama hiyo haitoshi, mabadiliko hayo yamekuwa yakienda sambamba na kubadilishwa kwa benchi nzima la ufundi, jambo ambalo linahitaji muda wa kutosha kwa makocha kuwasoma vizuri wachezaji ili kujua nafasi zao sahihi, lakini pia na wao wakihitaji kuzoeana uwanjani.

Kwa mantiki hiyo, pamoja na kwamba uongozi wa Yanga ulieleza kwamba benchi jipya la ufundi chini Nabi, litapokea rasmi kijiti baada ya msimu kumalizika na sasa timu itaendelea kuwa chini ya Kaimu Kocha Mkuu, Juma Mwambusi, kama ikiwa hivyo kweli, ni jambo la kupongezwa, ingawa tunaona ni vigumu hilo kutokea.

Hata hivyo, bila kujali kwamba Nabi na wasaidizi wake watapokea kijiti hicho kwa sasa ama baada ya msimu kumalizika, Nipashe tunatanguliza tahadhari kwa Yanga, tukitaka kuona benchi hilo jipya la ufundi halipewi presha kubwa ya kutwaa ubingwa kwa sasa.


Tunatambua Nabi na wasaidizi wake wameikuta Yanga ikiwa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu baada ya kushuka dimbani mara 26 na kujikusanyia pointi 57, mbili mbele ya mahasimu zao, Simba iliyopo nafasi ya pili lakini ikiwa na michezo mitatu mkononi.

Na nafasi hiyo, Yanga inaweza kuipoteza leo endapo Simba itaibuka na ushindi dhidi ya Gwambina FC katika mechi itakayopigwa Uwanja wa Gwambina, Misungwi nje kidogo ya Jiji la Mwanza.

Hivyo, matarajio yetu makubwa ni kuona mashabiki, wanachama na viongozi wa Yanga wakipunguza msukumo wa timu yao kutwaa ubingwa msimu huu, na kuwaeleza makocha hao kuwa lengo lao kubwa ni kutaka kuona wakijenga timu ya ushindani kwa ajili ya msimu ujao.

Kwa kufanya hivyo, kutasaidia makocha hao kudumu kwa muda mrefu na hilo likitokea, Wanayanga watashuhudia wakiwa na timu nzuri ya kutoa ushindani wa ubingwa wa ndani na kimataifa kama ilivyo kwa watani zao, Simba msimu huu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Angurumapo simba mcheza ni nani?

Na Barnabas Maro

NI mnyama gani anayeweza kucheza angurumapo simba, mfalme wa nyika? Methali hii huweza kutumiwa kuwapigia mfano watu wanaomdharau kiongozi au mkubwa lakini hujikunyata mara atokeapo.

Hata hivyo "Ana nchi yake simba, ana mji wake mamba," yaani simba huwa mfalme nchi kavu kama mamba alivyo mfalme majini. Methali hii hutumiwa kueleza mtu hawezi kuwa mzuri au kiongozi kila mahali. Kuna kwingine ambako wengine wanamzidi kwa ujuzi na uwezo.

Pamoja na yote, pia Wahenga walisema: "Anayejitahidi hufaidi" wakiwa na maana kuwa yeyote anayetia bidii hufaidi kutokana na juhudi zake. Methali hii inawasihi watu wawe na bidii katika shughuli yoyote waifatanyo.

Hapa sielezi mambo ya simba mnyama bali naeleza mambo ya Klabu ya Simba ambayo hata Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Sheikh Amani Abeid Karume (Mungu amrehemu) alipofungua jengo la Klabu ya Simba pale Msimbazi na kuambiwa klabu hiyo itaitwa "Simba" badala ya ' Manchester' alishituka na kuguna" " He! Simba? Haya."

Simba Sport Club iliyoundwa upya mwaka 1936 baada ya kutengana na Yanga mwaka 1935, ndio ninayoizungumzia. Hapana shaka ndio itakayokuwa klabu ya kwanza Ukanda wa Afrika ya Mashariki kutwaa Kombe la Mabingwa wa Afrika msimu huu, Inshallah (apendapo Mwenyezi Mungu.)

> **Hapana shaka ndio itakayokuwa klabu ya kwanza Ukanda wa Afrika ya Mashariki kutwaa Kombe la Mabingwa wa Afrika msimu huu, Inshallah (apendapo Mwenyezi Mungu.)**

Naomba wanachama wenzangu wa Yanga wasidhani nimehamia Msimbazi, hasha, (sivyokabisa!) Nilijiunga na Yanga tangu tarehe 2/12/1966 kwa kadi yenye namba 447 na picha ya mwenge wa uhuru wa Tanganyika na kupewa jina la utani kuwa "Mkono wa Kilambo" aliyekuwa beki mahiri wakati ule na baadaye kuwa kocha aliyeiwezesha Yanga kuifunga Simba mabao 5-0.

Sasa Simba si ile ya zamani kwa jinsi ilivyoimarishwa na Mohamed "Mo" Dewji. "Bahati ina miujiza, lakini haina ahadi." Maana yake kwa kawaida bahati huweza kuleta mambo ya ajabu lakini haitabiriki! Ni vigumu kuitabiri bahati. Methali hii inatumiwa tujitahidi bila kutegemea miujiza.

Yafaa tujikumbushe kuwa "Hasama ndimi za moto." Hasama ni uadui. Maana ya methali hii ni uadui au adawa ni kama ndimi za moto ambazo huchoma. Methali hii inatuhimiza tujiepushe na uadui ambao unaweza kutuletea maangamizo makubwa.

Leo naandika kimethali zaidi. "Wa kuume haukati wa kushoto." Maana yake mkono wa kuume haukati wa kushoto. Hii ni methali ya kutumiwa kutukumbusha kuwa watu wanaohusiana kama ndugu au jamaa hawawezi kudhuriana kwa urahisi.

Kwa bahati mbaya sana Yanga na Simba hudhuriana mojawapo inapocheza na timu ngeni inayotoka ughaibuni! Pukachaka! (Neno lenye kuashiria kutema mate linalomaanisha kukidharau kitu kilichotajwa.)

Methali zifuatazo zazihusu Simba na Yanga: "Ukijidhani umesimama uangalie usianguke" Maana yake udhaniapo umesimama unapaswa kuangalia usianguke. Methali hii huweza kutumiwa kwa mtu anayejitapa kutokana na hali nzuri aliyonayo, mathalani ya kiuchumi. Anapaswa kutambua kwamba hali hiyo yaweza kumwondokea na akabaki kama mwanzoni.

Kwa upande mwingine huwaambia: "Ukikosa shukuru, kupata kuna Mungu." Ukosapo kitu mshukuru Mungu tu kwani ndiye mwenye uwezo wa kutoa. Methali hii hutumiwa kuwanasihi watu wasiwe na tabia ya kulalamikalalamika. Mungu ndiye mwenye uwezo wa kila kitu.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

## HABARI BUNGENI

# Wanachama NSSF walipwa mafao bil. 378/-

**Habari zote na Augusta Njoji, DODOMA**

KATIKA kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, mwaka huu, wanachama 93,861 wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), wamelipwa mafao mbalimbali yenye thamani ya Sh. bilioni 377.8.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Vijana, Kazi na Ajira, Patrobas Katambi, alisema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Amina Hassan.

Katika swali lake, mbunge huyo alitaka kujua ni lini serikali itaondoa tatizo la ucheleweshaji wa malipo ya mafao kwa wastaafu wanachama wa NSSF.

Akijibu swali hilo, Katambi alisema serikali imekuwa ikihakikisha wastaafu wote wanalipwa mafao yao ya pensheni kwa mujibu wa Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pindi wanapostaafu.

"Ili mstaafu aweze kulipwa mafao ya pensheni ni lazima awe amekidhi vigezo ambavyo ni kutimiza umri wa kustaafu kwa mujibu wa sheria ambao ni miaka 55 hadi 59 kwa hiari na miaka 60 kwa lazima na awe amechangia kwenye mfuko kwa kipindi kisichopungua miezi 180 au miaka 15,"alisema.

Katambia alisema NSSF wastaafu wote wanaokidhi vigezo na kuwasilisha taarifa zote zinazohitajika hulipwa mafao ya pensheni kwa wakati pasipo kuchelewa.

Alisema mwanachama akiliwasilisha maombi ya kutaka kulipwa mafao na nyaraka husika zikikamilika, atalipwa mafao yake ndani ya siku 30.

"Malipo ya pensheni ya kila mwezi kwa wastaafu hulipwa tarehe 25 ya kila mwezi moja kwa moja kwenye akaunti za wastaafu na hadi sasa hakuna malimbikizo yoyote ya mafao ya pensheni kwa wastaafu," alisema.

Alitoa wito kwa waajiri kuwasilisha michango ya watumishi wao kila mwezi kwa wakati na wastaafu kuhakikisha wanawasilisha nyaraka zote zinazotakiwa kwa wanachama ili kuwezeshwa kulipwa mafao na kuondoa ucheleweshaji unaoweza kujitokeza katika kuandaa mafao ya wastaafu.

Hata hivyo, Naibu Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson, alishauri kuangaliwa upya kanuni ambazo zimekuwa kikwazo kwa wastaafu kwa kuwadai nyaraka ambazo ziliwasilishwa awali kabla ya kustaafu.

Akitoa ufafanuzi kuhusu hilo, Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Jenista Mhagama, alisema ofisi yake imekuwa ikifanya uhakiki wa waastaafu na moja ya matatizo ni wastaafu wanasumbuliwa kupeleka nyaraka na wakati mwingine kutakiwa kufanya hivyo wakati wameshastaafu.

# Serikali yaahidi kutafuta soko la asali

SERIKALI imesema itaendelea kuhakikisha upatikanaji wa soko la mazao ya nyuki kupitia mradi mpya wa kusaidia mnyororo wa thamani wa ufugaji nyuki utakaotekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2021/22.

Naibu Waziri Maliasili na Utalii, Mary Masanja, alisema jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Jackline Kainja.

Kainja, katika swali hilo, aliihoji serikali ni lini italiangalia zao la asali na kulitafutia soko la uhakika ndani na nje ya nchi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Masanja alisema kwa sasa uzalishaji wa asali nchini ni wastani wa tani 30,400 na sehemu kubwa ya asali hiyo huuzwa katika soko la nchini.

"Asilimia tano huuzwa kwenye soko la nje kwenye nchi za Rwanda, Kenya, Burundi, Umoja wa Jumuiya ya Ulaya na Umoja wa Nchi za Kiarabu,"alisema.

Aidha, alisema serikali imeweka mfumo wa ufuatiliaji wa mazao ya nyuki katika mnyororo mzima wa thamani wa mazao hayo kwa lengo la kudhibiti viwango vya ubora wa mazao ya nyuki, kufufua na kuendelea kuhamasisha uanzishwaji wa vyama vya ushirika wa wafugaji nyuki ili kuunganisha nguvu ya uzalishaji na kupata soko la uhakika.

Hata hivyo, alisema serikali inaendelea na ukarabati pamoja na ujenzi wa viwanda vya kuchakata mazao ya nyuki katika mikoa ya Tabora, Katavi, Kigoma na Geita ambavyo vitatumika kama soko la mazao ya nyuki.

# Mikakati kudhibiti homa ya nguruwe yawekwa bayana

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imeainisha mikakati minane iliyofanyika kudhibiti mlipuko wa ugonjwa wa homa ya nguruwe uliojitokeza hivi karibuni katika mikoa kadhaa na kusababisha hasara kwa wafugaji.

Naibu Waziri Abdallah Ulega, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Ndanda (CCM), Cecil Mwambe.

Mwambe alihoji mkakati wa serikali kuhakikisha kuwa mlipuko wa magonjwa ya Nguruwe haujitokezi mara kwa mara nchini.

Ulega akijibu swali hilo, alisema ugonjwa huo unaosababishwa na virusi, hauna chanjo wala tiba na kwamba njia pekee za kudhibiti ni kuzingatia kanuni bora za ufugaji wa nguruwe.

Alibainisha kuwa serikali na wadau wengine inafanya jitihada za kudhibiti ugonjwa huo ambazo ni pamoja na kuhimiza wafugaji kuacha kufuga nguruwe kwa njia huria, kuzuia wageni kuingia kwenye mabanda ya nguruwe.

Pia mkakati mwingine ni kuhimiza wafugaji wapulizie dawa za kuua virusi na kupe kwenye mabanda na kuweka dawa ya kuchovya kwenye milango ya mabanda, kuweka katazo la kusafirisha nguruwe na mazao yake kutoka sehemu zenye ugonjwa.

"Kuhimiza wafugaji kutokuruhusu wachinjaji au wafanyabiashara kuingia katika mabanda na kuchagua nguruwe wa kununua, wafugaji kuepuke kulisha nguruwe mabaki ya vyakula kutoka kwenye hotelini na migahawa,"alisema.

Nyingine ni kuacha kuchanganya nguruwe wageni na wenyeji kwenye banda moja na wafugaji kutoa taarifa za ugonjwa au vifo vya nguruwe pindi inapojitokeza kwa Mtaalamu wa Mifugo aliye karibu.

Hata hivyo, alisema mkakati wa serikali kupitia Wizara ni kuendelea kutoa elimu ya udhibiti kwa wadau wote katika mnyororo wa thamani, wakiwamo wafanyabiashara na wasafirishaji wa nguruwe pamoja na watoa huduma za afya ya mifugo.

"Kazi hii tunaendelea kuifanya kwa kuzingatia uhalisia katika kila eneo kwa wafugaji wakubwa na wadogo," alisisitiza.


SANTANA INVESTMENT LTD

SANTANA INVESTMENT LIMITED
Off Shekilango road, Sinza Kwaremi Muungano street, Plot B No. 335
P.O. Box 19944 DSM, E-mail: santanainvestment@yahoo.com Tel; +255787715057 +255713320653
Court Broker, Process server, Debt Collector, Tax Matters, Levies and Auction Mart
Reg Na. 114856 TIN Na. 126-205-929

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**KWA IDHINI TULIYOPEWA NA BENKI YA NBC, SISI KAMPUNI YA MADALALI WA MAHAKAMA YA SANTANA INVESTMENT LTD, TUTAUZA MALI/DHAMANA KWA NJIA YA MNADA KAMA IFUATAVYO:-**

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | MAELEZO YA DHAMANA | MADHAMA ILIPO | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Nashoni M.Nyamhanga | NYUMBA | CT NO.114412, PLOT NO.1047 BLOCK E TEGETA AREA DAR I.N.O JAMES POLISI. | TEGETA - DSM | 12/05/2021 SAA 08:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| 2 | Kinson Enterprises C | NYUMBA | plot no 267 block "Q4" kibamba area, kinondoni | KIBAMBA | 18/05/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 3 | Sospeter N Msuya | NYUMBA | Plot no 144 uyaoni area, kibaha township | KIBAHA | 20/05/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 4 | Zedeck Joseph | NYUMBA | CT NO.10179-MBYLR, L.O. NO.185601, PLOT NO.134, BLOCK 'F' MAKAMBAKO URBAN AREA,NJOMBE DISTRICT. I.N.O. | MAKAMBAKO URBAN | 25/05/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 5 | Egdi Gwido Sanga | NYUMBA | CT NO. 11984-MBYLR ,L.O.NO. 185792,PLOT NO. 164,BLOCK 'K' MAKAMBAKO URBAN AREA I.N.O EGIRD GWIDO SANGA | MAKAMBAKO AREA | 25/05/2021 SAA 08:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| 6 | Justin S Kapanga | NYUMBA | TITLE DEED OVER CT NO 11979 MBYLR PLOT NO 135 BLOCK F MAKAMBAKO LO NO 185655 IN THE NAME OF JUSTINE KAPANGA | MAKAMBAKO AREA | 26/05/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 7 | HASSAN JOSEPH LUKANKA | NYUMBA | CT NO. 033054/154, LO NO. 135154, PLOT NO. 103, BLOCK 'AA' MABATINI, MWANZA MUNICIPALITY i.n.o HASSAN JOSEPH | MABATINI AREA , MWANZA CITY | 01/06/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 8 | MUSSA MAIGE NYODA | NYUMBA | I CT NO 5936 LO NO 122073 PLOT NO 4 BLOCK EE NGOKOLO SHINYANGA I.N .O RAPHAEL OLAL ARIRO | NGOKOLO SHINYANGA | 04/06/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 9 | Silamu M Ganha | NYUMBA | CT NO 11523, PLOT NO.65 BLOCK JJ NDEMBEZI SHINYANGA MUNICIPALITY I.N.O GERASE BALIMUJURA RUKUMBERWA. SQUARE METRES 447 | NDEMBEZI SHINYANGA | 04/06/2021 SAA 08:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| 10 | Charles M. Mahushi | NYUMBA | CT NO.224888-LR MWANZA, L.O. NO.198481, PLOT NO.609 BLOCK 'HH' (HIGH DENSITY) NDOLA AREA I.N.O MBOJE NGASSA. SQUARE METRES 442 | NDALA AREA-SHINYANGA | 05/06/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 11 | Hamis Kombo | NYUMBA | CT.NO. 35430-LR MWANZA, L.O NO. 423417 , PLOT.NO. 36, BLOCK 'GG' SERVICE INDUSTRY,KITANGIRI AREA, SHINYANGA MUNICIPALITY I.N.OMAHONA. SQUARE METRES 600 | KITANGIRI - SHINYANGA | 05/06/2021 SAA 08:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| 12 | Sitta John Malubalo | NYUMBA | CT.NO.25874 LR, PLOT.NO. 377, BLOCK 'A' HD, SIMA, BARIADI URBAN AREA | SIMA-BARIADI | 07/06/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 13 | Mashaka Sengo Nyadu | NYUMBA | CT NO.36584-LR MWANZA, L.O NO.223800, PLOT NO.50 BLOCK 'B' MWAKIPUGILA AREA ,MEATU DISTRICT I.N.O MASHAKA SENGO NYANDU. SQUARE METRES 450 | MWAKIPUGILA AREA ,MEATU | 11/06/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 14 | Frida Furniture | NYUMBA | C.T NO. 20703 LR MWANZA L.O NO. 156243 PLOT NO. 320 BLOCK 'V' I.N.O JUVENALI SHABANI SHILYANGA, REGISTERED TO COVER AN UNSPECIFIED. SQUARE METRES 1,888 | NZEGA-TABORA | 14/06/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 15 | Twahiru H Semtindi | | C.T.NO.23363-LR MOSHI, L.O. NO. 171445, PLOT .NO. 1116, LUKOZI AREA, LUSHOTO DISTRICT I.N.O SHAURI ATHUMANI SEMTINDI. SQUARE METRES 22,200 | LUKOZI TANGA | 24/06/2021 SAA 08:00 MCHANA NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi anatakiwa kulipa 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada na kiasi kilichobaki cha 75% kilipwe ndani ya siku 14 toka tarehe ya kufanyika mnada, kinyume cha hapo kiasi kilicholipwa awali hakitarudishwa na mnada kufanyika upya.
2. Ukaguzi wa dhamana (nyumba au gari) utafanyika toka siku ya tangazo hili na gharama za ukaguzi na kuona dhamana hiyo ni za mteja mwenyewe.
3. Gharama za kubadili umiliki (transfer) ni za mteja mwenyewe.
4. Mnada utafanyika mahala dhamana zilipo.
5. Kwa maelezo zaidi wasiliana na Mkurugenzi Mkuu wa Santana Investment Ltd.

**Kwa mawasiliano mengine tafadhali piga namba zifuatazo:**
**0713-320653 / 0715-655950 / 0767-531622 / 0782-375475**

# Kaduma mwenyekiti sekretarieti ya ajira

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameemteua Katibu Mkuu Mstaafu wa Wizara ya Kilimo, Sophia Kaduma, kuwa Mwenyekiti wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.

Taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Gerson Msigwa, ilisema uteuzi wa Kaduma ulianza jana.

Uteuzi huo ni mwendelezo unaofanywa na Rais Samia katika kujaza nafasi mbalimbali za uongozi tangu aliposhika wadhifa huo machi 19, mwaka huu, baada ya kifo cha aliyekuwa Rais, Hayati Dk. John Magufuli. Mbali na Kaduma, Rais Samia pia amemteua Dk. Hedwiga Swai kuwa Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania. Dk. Swai anashika wadhifa huo kwa kipindi cha pili baada ya kipindi cha kwanza kumalizika.

Juzi, Rais Samia aliwateua watu mbalimbali kushika nyadhifa kadhaa. Miongoni mwa walioteuliwa ni Prof. Henry Fatael Mahoo kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

Pia alimteua Jaji wa Mahakama ya Rufani, Dk. Gerald Ndika, kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi la Chuo cha Uongozi wa Mahakama (IJA) Lushoto kwa mara ya pili baada ya kipindi cha kwanza kumalizika.

Pia aliwateua Prof. Aurelia Kamuzora kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Kahawa Tanzania na Prof. Idris S. Kikula kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Madini Tanzania na Prof. Abdulkarim Mruma na Janeth Lekashingo kuwa wajumbe wa Tume ya Madini Tanzania.

# Ubelgiji yaipa Tanzania bil 33/-

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Tanzania imepokea nyongeza ya Euro milioni nne kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji mkoani Kigoma kutoka Ubelgiji.

Hafla fupi ya utiaji saini wa mkataba wa marekebisho ya nyongeza ya mradi huo ilifanyika jijini Dodoma kati ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, kwa upande wa serikali na Balozi wa Ubelgiji nchini, Peter Van Acker.

Akizungumza katika hafla hiyo, Tutuba alisema mradi huo ambao ulianzishwa kwa ajili ya wilaya zote sita za Mkoa wa Kigoma, mwanzoni ulitarajiwa kugharimu Euro milioni nane.

"Sasa hizi Euro milioni nne zitakwenda kuongezea na kufanya jumla ya Euro milioni 12 sawa na takribani Sh. bilioni 33 za Kitanzania ambazo zitatumika kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa maji maeneo ya vijijini na mijini mkoani humo", alisema.

Tutuba alisema katika Mkoa wa Kigoma, Serikali ya Ubelgiji pia imefadhili mradi mwingine wa kilimo ambao unaendelea na umegharimu Euro milioni nane (Sh. bilioni 22).

SAGCOT
SOUTHERN AGRICULTURAL GROWTH CORRIDOR OF TANZANIA

**KUPOTEA KWA CHETI CHA USAJILI**

Taasisi ya Mfuko wa **SAGCOT (SCTF)** yenye Makao yake Makuu mjini Dar es salaam, inatangaza kupotelewa kwa cheti chake chenye usajili Namba **4174** maeneo ya Dar es salaam kilichotolewa na Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini **(RITA)** Mwaka **2011.**

**SCTF** inaomba yeyote atakaekiona akiwasilishe kwenye ofisi zetu zilizopo katika Jengo la Mpingo barabara ya Nyeyere Dar es salaam au kituo chochote cha polisi kilichopo karibu nawe kumbukumbu namba **DAR/KIL/RB/206768/2021.**

Pia waweza kuwasiliana nasi kwa simu namba **0754 288 278** au barua pepe: **jkyaruzi.emobile@gmail.com**

**SAGCOT Catalytic Trust Fund**
**Jengo la Mpingo- Barabara ya Nyerere**
**P.O Box 10977**
**DAR ES SALAAM**




Ofisa Mkuu wa Fedha Benki ya NMB, Juma Kimori (wa pili kushoto), akikabidhi tiketi ya ndege kwa mshindi wa droo kuu ya MastaBata 'Si Kikawaida', Indra Pratap, jijini Dar es Salaam juzi, ambaye ameshinda safari ya kutembelea Mbuga ya Serengeti pamoja na mwenza wake ikiwa imelipiwa kila kitu. Wengine ni Meneja Mwandamizi Biashara ya Kadi wa benki hiyo, Manfred Kayala (kulia) na Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard (katikati). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makandarasi wazalendo waiangukia serikali kupatiwa miradi ya ujenzi

**Na Joseph Mwendapole,**
MBEYA

MAKANDARASI wazalendo wameiangukia serikali wakiomba wapewe zabuni nyingi za ujenzi ili kukuza mitaji na kushindana na kampuni za kigeni.

Waliyasema hayo jana jijini hapa wakati wa mkutano wa siku mbili ulioandaliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) kwa makandarasi wa Nyanda za Juu Kusini.

Mkutano huo unaowashirikisha zaidi ya makandarasi wazalendo 300, ulifunguliwa jana na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leonard Chamuriho

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mabondi Electrical Contractors, Anania Mwakibete, alisema utaratibu wa serikali kufanya miradi ya ujenzi yenyewe kwa kutumia mfumo wa 'force account' umedidimiza uchumi wa kampuni za makandarasi wazalendo

Alisema miaka ya hivi karibuni, kulijengeka utaratibu wa miradi mingi ya serikali kufanywa na taasisi zake kama SUMA JKT kwa maelezo kuwa makandarasi binafsi wamekuwa wakichelewesha kukamilisha kazi au kutoza fedha nyingi.

Mwakibete alisema hata taasisi za umma zinazopewa zabuni na serikali nazo zimekuwa zikitekeleza miradi kwa fedha zinazolingana au kukaribiana na zile za makandarasi binafsi kutokana na gharama za ununuzi wa malighafi za ujenzi.

"Tunaomba serikali hii ifikirie kuturudishia kazi zetu, isiue ujuzi wetu ukiangalia makandarasi wengi tuna hali mbaya kiuchumi, sisi na familia zetu na wengine wamekopa benki wameshindwa kurejesha kutokana na uhaba wa kazi," alisema

Mkurugenzi wa Videfca Construction ya Iringa, Vitus Mushi, alisema makandarasi hawakatai baadhi ya miradi kutekelezwa kwa mfumo wa 'force account' lakini isichukuliwe kuwa makandarasi wazawa hawawezi.

Alisema mara kadhaa makandarasi wazalendo wamekuwa wakilalamikiwa kwamba wanachelewesha miradi hata wakati mwajiri ameshindwa kulipa fedha kwa wakati lawama zinawaangukia wao.

"Sisi tunakaguliwa mara kwa mara na kutoa vyeti vya kazi mahali tulipofikia kitu ambacho hatudhani kwamba kinafanyika kwenye utaratibu wa 'force account', halafu wao wanaletewa malighafi zote eneo la kazi kama nondo, mchanga, kokoto, sarufi wakati sisi tunatafuta wenyewe wakati mwingine mbali na malipo yanachelewa wakati mwingine," alisema

Alisema makandarasi wengi walikuwa wakilaumiwa kuchelewesha miradi ya maji lakini ukweli ni kwamba watoa kazi wengi ndio walikuwa wakichelewa kutoa fedha za utekelezaji wa miradi husika.

"Unakuta kiongozi anakuja anahoji mbona mradi haujakamilika na bila kujali sababu zilizochelewesha mradi. Anaamuru utaratibu wa 'force account' utumike, mradi unaweza kufanywa haraka lakini usiwe na kiwango. Ukichunguza miradi mingi ya 'force account' inajengwa haraka haraka. Tujiulize ina ubora kama miradi yetu?" alihoji.

Edna Kajiba ambaye ni Mkurugeni Mtendaji wa Kampuni ya Shahazuru alisema ni matarajio yake kuwa serikali mpya itasikiliza kilio cha makandarasi wazalendo ili kuwapa kazi nyingi zitakazosaidia kuimarisha mitaji yao.

"Sisi makandarasi wazalendo tunaamini kwamba Rais wetu atasikiliza kilio chetu ili tupewe kazi na tuwe tunalipwa kwa wakati ili tukamilishe miradi husika kwa wakati kwasababu usipolipwa kwa wakati huwezi kukamilisha kazi kwa wakati," alisema



**HABARI DODOMA**

# Waagizwa kufanya uchaguzi haraka

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BARAZA la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NACoNGO), limeagizwa kufanya uchaguzi wa viongozi kwa mujibu wa sheria ili kutimiza majukumu yake kisheria.

Mwenyekiti wa Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Dk. Richard Sambaiga, alitoa maelekezo hayo jana katika Kikao cha 46 cha Bodi ya Mashirika hayo jijini hapa.

Alisema NACoNGO imekuwa ikiomba kuongezewa muda mara kwa mara jambo ambalo limefika mwisho na kutaka kuhakikisha inakamilisha uchaguzi wa viongozi wake kabla ya Juni Mosi, mwaka huu, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa matakwa ya kisheria.

Dk. Sambaiga alisema bodi hiyo ipo kwa mujibu wa sheria, ina mamlaka ya kuhakikisha utekelezaji wa Sera ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Kanuni na utendaji kazi wa NACoNGO ikiwa pamoja na kufanyika kwa uchaguzi wa viongozi wa baraza hilo.

"Tulishatoa agizo la kwanza Machi 31, 2020 kufanya uchaguzi kuchagua viongozi wenu ndani ya kipindi cha miezi minane lakini hamkutekeleza hilo, ... mmekuwa mkiomba kuongezewa muda na hadi sasa mnaomba kupewa muda zaidi," alisisitiza.

Alifafanua kuwa Machi 3, 2021 Bodi iliongeza muda wa siku 14 kutekeleza maagizo hayo lakini bado agizo hili halikutekelezeka.

Awali, akitoa maelezo kuhusu utekelezaji wa maelekezo ya bodi, Kaimu Katibu Mkuu wa NACoNGO, Focus Magwesela, alisema baraza hilo linashindwa kukidhi matakwa ya sheria kutokana na uhaba wa rasilimali fedha.

Aliomba kuongezewa miezi mingine mitano ili kutekeleza maelekezo hayo.

**"Tulishatoa agizo la kwanza Machi 31, 2020 kufanya uchaguzi kuchagua viongozi wenu ndani ya kipindi cha miezi minane lakini hamkutekeleza hilo, ... mmekuwa mkiomba kuongezewa muda na hadi sasa mnaomba kupewa muda zaidi," alisisitiza.**

# Sababu ongezeko VVU Misungwi zatajwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa miongoni mwa mambo yanayochangia maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) katika Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza ni pamoja na ndoa za ututoni, kurithi wajane na kuchanja chale kwa kuchangia wembe.

Mambo hayo yaliibuliwa mwaka jana katika tathmini ya kitaifa juu ya mwitikio wa udhibiti wa VVU iliyofanywa na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wanawake (UN-Women) na Shirika la Umoja wa Mataifa linalojishughulisha na UKIMWI (UNAIDS).

Akizungumza jana jijini hapa katika mafunzo yaliyotolewa na serikali kupitia TACAIDS kwa ufadhili wa mfuko wa Global kwa uwezeshaji kutoka UN-Women, Mratibu wa Programu za UKIMWI na Jinsia kutoka UN-Women, Jacob Kayombo, alisema tathmini hiyo ilizingatia vipaumbele vya jinsia. Alisema jamii ya Misungwi ilieleza mila potofu ambazo zimekuwa zikichangia maambukizi hayo.

Alisema kwa sasa wako katika hatua za maandalizi ya kupanga kazi lakini kuangalia mikoa gani ambayo wataifikia kutokana na vipaumbele ambavyo viliainishwa katika tathmini hiyo ikiwamo kutoa elimu kwa jamii kuondokana na mila potofu.

"Kwa mfano tunaposema ndoa za ututoni zinakuwa si za hiari bali ni za lazima. Kwa hiyo anayelazimishwa haki zake kama binadamu zinakiukwa na mbali na kukiukwa, huyu anayelazimishwa anawekwa kwenye hatari ambayo mwisho wa siku inaweza kuwa na madhara," alisema.

Alisema mikakati iliyopo ni kutoa elimu kwa viongozi wa mila na desturi ambao wao ndio wenye kauli katika kutekeleza mila hizo.

"Tunawaelimisha wajue uzuri na ubaya wake lakini tunawafanya waone kuwa wana wajibu katika makundi wanayoongoza ili kubadilika," alisema huku akiitaka jamii izingatie kuna mila zinakinzana na hali halisi ya masuala ya afya ya jamii.

Hata hivyo, aliitaka jamii itambue kuwa bado kuna sheria ya kuwalinda wanawake na wasichana kama ilivyo kwa makundi mengine katika jamii.

Naye Mratibu wa Masuala ya Jinsia kutoka TACAIDS, Judith Luande, alisema mafunzo hayo wezeshi yametolewa kwa wataalam ambao wataenda katika ngazi ya halmashauri kufundisha wengine kwenye jamii ili kuondoa mila hatarishi zinazosababisha maambukizi hayo.

"Kuna wakati tulifanya tathmini ya masuala ya UKIMWI na mtazamo wa kijinsia na utekelezaji wake Misungwi ni mojawapo ya halmashauri tuliyoifanyia na masuala ya mila hatarishi yanafanyika kwa kiasi kikubwa," alisema.

Mratibu wa Kudhibiti UKIMWI Misungwi, Dk. Marcelina Kiemi, alisema tatizo kubwa linalolikumba eneo hilo ni ndoa za ututoni ambapo mabinti wanaozeshwa wakiwa na umri mdogo kwa watu wenye umri mkubwa.

"Kingine kilichopo katika wilaya yangu ni mila na desturi ya kurithi wajane unakuta pengine hajapima virusi hajajua hali yake anakuta anampelekea yule mwanamke," alisema.

Pia alitaja matibabu ya kijadi ambayo yamekuwa wakichangia vifaa vyenye ncha kali kuchanja chale yanachochea maambukizo.



Meneja wa Shamba la Silverlands la Ifunda mkoani Iringa, Wayne Travis (kulia), akitoa maelezo kuhusu umwagiliaji wa kitaalam kwa wanafunzi wa Chuo cha Kilimo cha Mt. Maria Goretti, ambao ni wanufaika wa programu ya ufadhili wa masomo wa kampuni ya SBL, unaojulikana kama "Kilimo Viwanda", walipotembelea shamba hilo mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbunge alilia nyongeza bajeti TARURA

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kuangalia bajeti ya Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) Wilaya ya Kishapu kwa jicho la pekee ili itekeleze majukumu yake ipasavyo.

Hali hiyo inatokana na maeneo mengi vijijini kukabiliwa na ubovu wa barabara na hivyo kusababisha wakulima kushindwa kusafirisha mazao yao.

Akizungumzia hali hiyo jana, Mbunge wa Kishapu (CCM), Boniphace Butondo, alisema kiwango ambacho TARURA inatengewa kwa ajili ya barabara ni kidogo.

"Eneo la Kishapu tuna kilomita 1030 zinahitajika kutengenezwa kuna maeneo yapo kwenye mbuga vile ni vijiji na kuna maeneo ya utawala kwa vyovyote vile huduma ya barabara ni muhimu ili kurahisisha wananchi kuzifikia huduma," alisema.

Butondo alisema kuna wakati wanafunzi wanashindwa kwenda shuleni kutokana na barabara kujaa maji.

"Pia ni tatizo kwenye usafirishaji wa mazao, Mkoa wa Shinyanga unalima sana pamba lakini Wilaya ya Kishapu ndiyo inayoongoza kwa kulima pamba. Pamoja na hayo wanaongoza kwa kukabiliwa na tatizo la barabara. nashauri serikali kuongeza fedha na kutengeneza barabara Wilaya ya Kishapu."

"Ikinyesha tu mvua safari ya kwenda Kata za Itilima, Kilolei, Mwamalasa hizi ni kata hazipitiki kabisa tusipoangalia tutakatisha tamaa wananchi, hili jambo tunaweza kuliangalia ili kuwafungulia njia wananchi kwa kuweka tozo kwenye simu au barabara," alisema.

Kuhusu upungufu wa walimu, alisema kuna upungufu wa walimu 1,611 na kwamba kuna tatizo kubwa.

"Kuja haja ya serikali kusaidia nguvu ya wananchi kwenye ujenzi wa shule za msingi na sekondari katika umaliziaji wa maboma," alisema.

Akizungumzia maslahi ya madiwani, Mbunge huyo alisema madiwani wanakabiliwa na shida kubwa kwenye suala la maslahi licha ya wao kuwa ni wasimamizi wa karibu wa miradi ya maendeleo na kushauri kuongezewa posho za madaraka.



# Askari waliompiga mwandishi kikaangoni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar, imeahidi kuwachukulia hatua askari wanne wa Kikosi cha Valantia (KVZ) waliodaiwa kumshambulia mwandishi wa babari wa gazeti la Mwananchi, Jesse Mikofu.

Mwandishi huyo alishambuliwa na askari hao katika eneo la Darajani Aprili 21, mwaka huu, akiwa katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mawaziri wa Habari, Vijana, Utamaduni Sanaa na Michezo, Tabia Maulid Mwita, na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Mohammed, walisema hayo jana kutokana na tukio la kupigwa kwa mwanahabari huyo. Akitoa kauli ya serikali, Waziri Masoud alisema serikali inayosimamia misingi ya haki na uadilifu kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na sheria zingine, haijaridhishwa na wala haikubaliani na tukio hilo na itahakikisha inachukua hatua kwa mujibu wa sheria kwa watu waliohusika na tukio hilo.

Masoud alisema serikali inalaani tukio hilo kwa kauli moja na si agizo walilopewa na serikali wala utamaduni wa chombo chochote cha ulinzi bali ni tukio lililofanywa na mtu asiye na maadili ya kazi na kutotambua mipaka ya shughuli zake.

Alisema tayari ameshatoa agizo kwa Kamanda Mkuu wa KVZ kuhakikisha anatoa orodha ya watendaji waliokuwapo katika eneo la Darajani siku hiyo ili kuwa rahisi kubaini askari waliofanya udhalilishaji huo.

"Wao walikuwa katika majukumu yao ya kazi hivyo hawakuwa na haki ya kuzuia wengine kutekeleza majukumu yao na waandishi walikuwa na haki ya kutekeleza wajibu wao kama walivyokuwa wao," alisema.

Alisema sheria inayoongoza KVZ kama chombo ikiwamo mahakama ya kijeshi itahakikisha inachukua mkondo wake ili kuona inatenda haki kwa pande zote.

Waziri Masoud alikiri katika vikosi hivyo si mara ya kwanza kufanya matukio hayo na jambo kubwa ni kutokuwa na nidhamu kwa baadhi ya watendaji na matukio mengine yanayokandamiza haki za watu kwa kutumia mabavu kwa vyombo vilivyopewa dhamana ya kulinda raia na mali zao.

Aliwahakikishia wanahabari kuwa tukio hilo haliwezi kuwa mwendelezo na kutoingiwa na hofu juu ya kutekeleza majukumu yao na badala yake kuendelea kushirikiana na serikali katika kutekeleza majukumu kwa mujibu wa sheria na miongozo ya taaluma yao.

Pia aliwaahidi wanahabari na wananchi kuwa serikali haitakaa kimya na baadaye itaeleza hatua zitakazochukuliwa juu ya watendaji hao kwa kuwajibika ipasavyo juu ya jambo hilo.

Naye Waziri Tabia alisema Zanzibar inaendeshwa kwa misingi ya kikatiba, kuheshimu uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa harakati za vyombo hivyo.

Alisema wizara inachukua juhudi mbalimbali kuhakikisha wanahabari wanapata haki zao na kutatua changamoto zao ili kuona wanahabari wanafanya kazi katika mazingira mazuri.

Waziri Tabia aliwahakikishia wanahabari kuwa wizara itaendelea kuwalinda, kulinda maslahi yao na mazingira yao ya kufanyia kazi.



Waumini wa Dini ya Kiislam wakiitikia dua iliyosomwa na Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kabi (hayupo pichani), wakati wa Sala ya Ijumaa iliyofanyika katika Masjid Al-Jalil Mbuzini Wilaya ya Magharibi A, Unguja na kuhudhuriwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dk. Hussein Ali Mwinyi. **PICHA: IKULU**

# Mfumo wawaondolea wafanyakazi msongo wa mawazo mahali pa kazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KUWAPO kwa mfumo mzuri wa usalama na afya kazini kunamjenga mfanyakazi kufanya kazi zake kwa weledi na kumwondosha katika msongo wa mawazo katika kazi

Hayo yalielezwa jana na Ofisa Msajili na Mkaguzi wa Sehemu za Kazi, Ame Faki Saleh, wakati akitoa mafunzo kwa wanafunzi na walimu wa vyuo Mbweni na Chuo Kikuu cha Sumeti, Chukwani.

Alisema iwapo mfanyakazi atawekewa mfumo mzuri wa kazi katika taasisi husika, atafanya kazi kwa uadilifu.

Wafanyakazi wengi hivi sasa, alisema wamekuwa wakikumbwa na msongo wa mawazo kutokana na sehemu wanazozifanyia kazi kutokuwa salama licha ya idara ya usalama kazini kuchukua jitihada kubwa za kuelimisha.

Alisema watu wengi wamekuwa wakikumbwa na msongo wa mawazo kutokana na mazingira yasiyo rafiki kwa wafanyakazi. Kutokana na hali hiyo, alisema idara ya kazi imekuwa na utaratibu wa kutembelea sehemu ambazo wafanyakazi wanafanya kazi serikalini na kampuni binafsi.

Alisema sheria ya kazi imebainisha kuwa mwajiri akitaka kumwajiri mfanyakazi kwa mwaka, lazima mwajiriwa achunguzwe afya yake ili kujulikana matatizo ya kiafya kabla hajaanza kazi.

Taasisi hiyo, alisema imekuwa na wigo mpana wa kuwasomesha wafanyakazi na waajiriwa ili kujua kanuni na sheria za usalama na afya kazini kwa sababu kuna baadhi ya taasisi katika sehemu za kazi haziko rafiki kwa wafanyakazi.

Alisema katika kipindi hiki cha kuelekea kilele cha usalama na afya kazini, idara imejipanga kuhakikisha wanafunzi wa vyuo vikuu kuwapa mafunzo ya afya kazini ili kujiandaa katika sehemu zao za kazi.

Naye Mkaguzi wa Usalama na Afya Kazini, Said Bakari Khamis, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuelimisha vijana wa vyuo na wako karibu kupata nafasi za kuajiriwa na kujua sheria za kazi na usalama na afya kazini.

Kwa mujibu wa mkaguzi huyo, taasisi inayosimamia usalama na afya kazini imepewa uwezo wa kukagua taasisi na kampuni mbalimbali ili kujiridhisha usalama wa wafanyakazi wa afya kazini wote wanapokuwapo kazini.

Alisema katika kufuatilia kazi zao, wanafanya kwa mujibu wa sheria bila kupendelea upande wowote kwa mujibu wa sheria .Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Sumeti, Mohammed Khalfan, alisema katika kufikia malengo ya sheria za usalama na afya kazini, lazima kwanza kufanyiwa marekebisho katika sheria ya idara ya kazi.

Alisema uhalisia kuwa sheria namba nane ya kazi iliyotungwa mwaka 2005 ilikuwa ina upungufu katika sheria hiyo.

# Kamati yawapa ujumbe watumishi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii ya Baraza la Wawakilishi, Ali Suleiman Ameir, amesema wakati utekelezaji wa mradi wa viungo ukiendelea, kuna haja watendaji kuhakikisha wanafanya kazi kwa moyo wa uzalendo ili ulete tija zaidi kwa wananchi na serikali kwa ujumla.

Aliyasema hayo jana wakati wa kikao maalumu katika ofisi za utekelezaji huo, Mwanakwerekwe, mjini Unguja, katika kikao kilichokuwa na lengo la majadiliano ya kufanya ushawishi wa kisera kuhusu sekta ya kilimo.

Alisema wakati mradi huo unatekelezwa watendaji wanapaswa kutambua kuwa wana wajibu wa kuhakikisha wanapata matokeo chanya ya mradi huo kinyume na miradi mingine ambayo imeshindwa kufanya vizuri.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, kuna haja ya kuhakikisha wanufaika wa mradi huo ni walengwa husika na si watu wengine.

"Lazima tutambue kuwa serikali ina matumaini makubwa na mradi huu kwa maslahi ya wananchi wake, hivyo lazima mfanye kazi kwa umakini sana," alisema.

Naye mtalamu wa masuala ya kilimo, Salum Rehani, alisema kuna haja kwa serikali kuweka utaratibu maalum wa utafiti ambao utasaidia kwa kiasi kikubwa kutambua mbegu bora za kilimo zinazopaswa kupandwa kulingana na mazingira husika.

Alisema serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kununua mbegu pamoja na mbolea lakini faida inayopatikana haiendani na uhalisia kutokana na hasara mbalimbali wanazokutana nazo wakulima.

"Ninaamini kuwa iwapo utafiti utafanyika tutakuwa na uhakika tunalima bidhaa gani, wapi na kwa muda gani na si watu kukurupuka tu. Kwa mfano unaona zao la nyanya linavyoshuka bei kwa kuwa watu wote wanalima wakati mmoja," alisema.

Meneja wa utekelezaji mradi huo Kanda ya Unguja, Khadija Juma, alisema Zanzibar ni sehemu iliyojaliwa fursa kubwa katika sekta ya kilimo na kwamba anaamini utekelezaji huo utaleta faida chini ya ushirikiano wa pamoja.

Aliwaomba wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuendelea kuishawishi serikali kutambua umuhimu wa kuwekeza zaidi katika kilimo kwa kuwa

**Alisema serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kununua mbegu pamoja na mbolea lakini faida inayopatikana haiendani na uhalisia kutokana na hasara mbalimbali wanazokutana nazo wakulima.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI APRILI 24, 20



MCHEKESHAJI ADA JESUS AAGA DUNIA Uk.14



## MIMI NI MWANAMKE

# Nikijipodoa wee acha tu

JE, umewahi kufikiria siku moja kumuona rapa mkali wa kike nchini, Chemical, amepigilia gauni au dera kama wanavyovaa wanawake wengine? Basi kabla hujapata jibu, yeye mwenyewe kaweka wazi kwamba suala hilo halitawezekana.

Akizungumza katika kipindi cha E News kinachorushwa na EATV, Chemical amesema hapendi kuvaa mavazi ya aina hiyo kwani anahofia kugombana na wenzake kwa kuwachukulia wanaume zao.

Amesema kwa sasa amechagua aina ya mavazi yanayomtofautisha na wengine, licha ya wengi kumjadili nguo hizo zipo sawa na wanaume.

"Napenda nguo ambazo hazipo kama mwanamume, zipo katikati, nikivaa nakuwa na utofauti na ndio mashabiki wangu wanapenda kuniona nikiwa hivyo," alisema.

Hata hivyo, amepingana na madai ya baadhi ya watu kwamba ana tatizo la kujiweka kama mwanamume, akieleza yeye ni mwanamke mzuri aliyekamilika na kuumbika.

Chemical amesema watu wasiuchukulie poa mwonekano wake kisa anafanya muziki wa HipHop, kwani akisema ajipodoe au apendeze kama wanavyofanya wanawake wengine basi itakuwa balaa kwa wanaume.

"Nikiamua kuvaa nitachukua mabwana wengi sana, ndiyo maana sitaki kukaa huko, mimi ni mzuri sana na nimeumbika kila kitu, siku nikiamua kujipodoa kama wanavyofanya wengine au wanavyovaa mtanipiga kwa sababu nitachukua vitu vyenu vingi na sipo tayari kugombana na watu" ameeleza.

BASI SAWA

## Diamond kawa baba mwenye busara

NI kauli ya baba mwenye busara! Ndivyo wiki hii msanii maarufu wa muziki wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz, alivyofanya baada ya kutoa kauli nzito inayobeba maana ya baba kwa watoto wake.


Diamond, ameamua kuingilia kati sakata la Harmonize kuwafikisha polisi baadhi ya wasanii akiwamo Rayvanny na Baba levo, akisema kinachoendelea sio kama alivyowalea ndani ya WBC.

Mwanamuziki huyo amesema hatua waliyofikia ya kufikishana polisi haimfurahishi kwani angependa kusikia wanashindana kwenye kazi.

"Sijafurahishwa kusikia wanapelekana Polisi, waige mifano ya sisi kaka zao mimi na Alikiba, hatukuwahi kuepelekana polisi tulikuwa tunashindana kupitia kazi zetu," amesema Diamond.



## Ebitoke ufupi una raha yake



MSANII wa vichekesho, Ebitoke amesema hakutaka kuingia katika shindano la Miss Tanzania 2020, baada ya kujitathmini na kugundua ufupi wake ungeleta usumbufu jukwaani.

Akizungumza na eNewz ya East Africa TV, Ebitoke amesema Kila mara alikuwa akijiangalia katika kioo na kugundua yeye ni mfupi na hawezi kuvaa viatu vyenye visigino virefu.

"Ulinishinda kwa sababu nilijiangalia kwenye kioo mara nyingi nikasema na ufupi huu nitaenda kuwa miss gani viatu virefu kutembelea shida, kiukweli nina kasura fulani hivi lakini sio fani yangu" amesema Ebitoke




## Shilole ndiyo kaolewa

WATANZANIA na wapenzi wa muziki wamepokea kwa furaha taarifa ya mwanamuziki na mjasiriamali, Zuwena Mohamed, maarufu kama 'Shilole' kuwa ameolewa na mpenzi wake Rajab Issa anayefahamika kama Rommy.

Juzi kupitia ukurasa wake wa mtandao wa Instagram, Shilole aliandika na kuthibitisha kwamba kafunga ndoa na Rommy ambaye amempita umri.

"Alhamdulillah tumemaliza salama, rasmi ni mke niliechukuliwa kwa furaha na upendo wa juu, kwa sasa unaweza kuniita Mrs Rajab Issa.. Yarabbi iwe salama".

Hata hivyo baadhi ya wafuasi wake wamemtaka mwanamuziki huyo kutulia na mume wake, kwani wamechoshwa na tabia yake ya kuwaacha waume zake katika mtindo wa aina moja.



## Shamsa ukisikia kudemka ndo huko!

MSANII mkongwe wa filamu nchini, Shamsa Ford, amejikuta akitoa dukuduku lake baada kumwambia mwigizaji mwenzake, Rose Ndauka, kuacha kuimba kwani hana sauti.

Shamsa amesema hakuna umuhimu wa kuingia katika fani ambayo imekutupa mkono, hivyo ni bora kuwaachia Maua Sama na Rosa Ree wenye vipaji vyao.

"Rose Ndauka anapenda kuimba sio kwamba hajui, anamuelekeo kidogo na muda utaongea zaidi ila kwangu mimi naona bado kabisa anisamehe kwa hili bora tuendelee kufanya 'movie', mpaka huu mwaka uishe tutaona mengi muziki tuwaachie wakina Maua Sama, Nandy na Rosa Ree" amesema.

## Kipofu; Mungu hakupi kilema, ukakosa mwendo

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mwingine dunia haiko salama kwa walimwengu wake, hasa wale wema. Kuna binadamu wapo duniani kwa ajili ya kuifanya kuwa uwanja wa fujo.

Kuna watu wanaotaka wafanye lolote lile duniani kwa sababu tu ya kuamini nguvu walizonazo.

Hebu tuiangalie filamu ya 'Kipofu'. Ni filamu yenye mafunzo inayoonyesha jinsi watu walivyo na roho mbaya kuliko wanyama.

Msichana mmoja aliyekuwa na begi kubwa alikuwa akifuatiliwa na watu nyuma. Baada ya kushtuka aliamua kufanya kila njia kuwaepuka wale watu aliowaona wana nia mbaya na kwenda kulificha porini.

Wakati akiamini kuwa kuko salama na kwenda kuuchukua mzigo wake porini. Anamaliza kuuchukua tu, anatokea na jamaa mmoja anayemuonyesha bastola na kuutaka mzigo ule.

Wakati msichana akishangaa na kutaka kuumkabidhi mzigo, jambazi huyo anapokea kipigo kikali kutoka kwa mtu mwingine.

Mtu huyo anamnusuru msichana huyo kupokwa begi lake. Hata hivyo anaachiwa huru bila kudhuriwa.

Msichana anakuja kugundua kuwa mtu aliyemsaidia ni kipofu na anaitwa Tonny. Kwa msaada huo anapewa kiasi cha Sh. Milioni mbili kama asante.


Tonny alipofika nyumbani na kumwonyesha kitita hicho mkewe, hakuamini kama kweli alipewa kwa kutoa msaada, bali huenda alihongwa na hawara yake. Ugomvi unaanza, kiasi cha kuifanya ndoa kuwa matatani, kitu ambacho kilimfanya kuwa na mpango wa kutaka kuzirudisha pesa hizo kwa mwenyewe.


Maharamia katika tafuta yao, wanagundua nyumbani kwa Tonny, yule aliyemzuia mwenzao kuchukua begi lililojaa noti.

Wakati Tonny hayupo, wakavamia nyumbani na kumteka mtoto wake, wakampiga vibao mkewe na kumpa sharti la kuleta pesa zilizopo kwenye begi ili mtoto aachiwe.

Tonny, kipofu ambaye pamoja na ulemavu alionao, amejaaliwa nguvu na Mwenyezi Mungu pamoja na yeye mwenyewe kujifunza sanaa za mapigano.

Kutekwa kwa mtoto wake kunamfanya kuingia rasmi kazini kukuokoa mtoto wake. Anafanya kazi kubwa ya kuliangamiza kundi zima la maharamia na kumuokoa mtoto wake, pamoja na msichana yule ambaye naye alikuwa ameshatekwa na kundi hilo kwa ajili ya kuzitaka tena zile pesa zilizokuwa kwenye begi. Tonny, alimwokoa mtoto wake, msichana na begi lake la pesa.





## Kolabo kali Wabongo, Wakongo

**Na Adam Fungamwango**

HABARI ya mjini kwa sasa ni msanii Harmonize kutoa vipande vya ngoma yake kali iitwayo 'Attitude' ambayo amemshirikisha mwanamuziki maarufu kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Awilo Longomba.

Wengi wanamkumbuka Awilo ambaye alitamba miaka ya nyuma akipiga 'drums' kwenye bendi za Loleto Group ikiongozwa na hayati Aurlus Mabele, Zipompapompa iliyokuwa ikiongozwa na Luciana Domingongo.

Awilo, ingawa si mara ya kwake ya kwanza kufika nchini, yupo Dar es Salaam, kukamilisha 'singo' hiyo.

Hii si mara ya kwanza kwa wanamuziki wa Kongo kushirikiana na wasanii au wanamuziki wa Tanzania kutoa nyimbo.

**Borabora Sound ft Madilu System-Elowa**

Mwaka 2002, mwanamuziki maarufu nchini Kongo, Madilu System ambaye alifariki mwaka 2007, alifika nchini Tanzania. Pamoja na kufanya maonyesho, alishirikiana na bendi ya Borabora Sound kutoka kibao kimoja kilichopendwa sana kiitwacho 'Elowa'.

Ukikisikia huwezi kuamini kuwa kilipigwa na wanamuziki wa Kitanzania. Madilu aliimba pamoja na mwanamuziki ya Kikongo anayeishi nchini, akipigia bendi za Zaita Musica na Kilimanjaro Connection, Delphin Mununga.

**Twanga Pepeta ft Bozi Boziana-Mapenzi**

Wimbo huu unaitwa 'Mapenzi Hayana Kiapo'. Ulitoka kwenye albamu ya 'Dunia Daraja' mwaka 2014 ya bendi ya African Stars 'Twanga Pepeta'. Ni wimbo ambao walimshirikisha mwanamuziki maarufu ya Kongo, Bozi Boziana. Ikumbukwe kuwa mzee Benzi amekuwa na uhusiano na mzuri na mmiliki wa bendi hiyo Asha Baraka, na hiyo haikuwa mara ya kwanza kuja nchini kwa mwaliko wa Twanga Pepeta. Bozi ambaye alitamba mwanzoni mwa miaka ya 1980 na wimbo wake wa 'Tembe na Tembe', aliwahi kufanya ziara nchini na kutoa wimbo uitwao 'Dar es Salaam' alioimba Kiswahili.

**Diamond ft Innoss B-Yope Remix**

Ilikuwa ni bonge la kolabo kati ya msanii wa kizazi kipya wa Tanzania, Diamond Platinumz na msanii wa muziki wa kizazi kipya nchini Kongo, Innoss B mwaka 2019.

Walitoa ngoma moja kali iitwayo 'Yope Remix'. Hii awali ilichezwa na Innoss, lakini walishirikiana na kutoa kolabo. Ni ngoma iliyotazamwa na zaidi ya watu milioni 149 kwenye mtandao wa kijamii.

**Diamond ft Koffi Olomide-Waah**

Mwishoni mwa mwezi Novemba, mwaka jana, msanii Diamond Platinumz alitoa ngoma yake aliyoiita 'Waah', akimshirikisha mwanamuziki asiyechuja nchini Kongo, Koffi Olomide.

Ni moja kati ya 'kolabo' bora kabisa iliyotikisa mwaka jana.

**Nandy ft Koffi Olomide-Leo Leo**

Koffi alirejea tena Tanzania kufanya 'kolabo'. Safari hii siyo na Diamond tena. Ila na msanii wa kike Nandy. Ilikuwa ni Februari mwaka huu, wakati aliposhirikishwa kwenye ngoma ya 'Leo Leo' ambayo iliwashika vilivyo wapenzi wa muziki wa dansi na hata kizazi kipya.



# Lil Wayne afunga ndoa

IMEFAHAMIKA kwamba rapa mkali kutoka Marekani, Lil Wayne, amefunga ndoa.

Kulingana na mashuhuda, mwanamuziki huyo amemuoa kwa siri mrembo kutoka Peurto Rico, Denise Bidot.

Kwa muda wa wiki kadhaa Lil wayne na mpenzi wake huyo walikuwa wakiposti video zikiwaonyesha wakila raha katika fukwe ya bahari.



## 2Face akomalia kitengo cha magonjwa

MWANAMUZIKI maarufu kutoka Nigeria, 2Face Idibia, amekitaka kitengo cha kuzuia magonjwa na dawa nchini humo kuiacha tabia ya kuwanyanyasa watu wanaojaribu kusafiri kwenda nje.

Staa huyo wa muziki ameandika ujumbe kupitia ukurasa wake wa Instagram, kuwa wafanyakazi wa kitengo hicho wana ujuzi duni na usio na mipaka.

Amesema watu wanaosafiri kupitia uwanja wa ndege wa Lagos, wanapata wakati mgumu kutokana na utaratibu mbaya unaofanywa na wafanyakazi wa kitengo hicho.

## Mery awakaba wanaume bahili

STAA wa uigizaji wa Nigeria, Mary Remmy\Njoku, amesema wanaume wa Kiafrika wanaamini kutoa pesa za matunzo kwa ajili ya wake zao ni kama msaada.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Mary amesema kwamba ndoa ni kama timu moja, ni lazima mwanamume awajibike kwa matumizi ya ndani,

"Wapendwa wanaume wa Kiafrika, huwezi kumfanyia chochote mke wako, mama wa watoto ni lazima kutoa pesa za matumizi, kufanya hivyo sio msaada ni wajibu wako,' amesema.





## Regina kweli umeongeza hipsi?

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Regina Daniel, inadaiwa kufanyiwa upasuaji wa kurekebisha viungo.

Mjadala mkali umeibuka katika mitandao ya kijamii, baada ya staa huyo kuposti video fupi katika mtandao wa Snapchat, akionekana yupo katika chumba cha upasuaji,


Video hiyo iliambatana na ujumbe unaosema ""Hello wapendwa nakwenda katika upasuaji, pembeni yangu kuna mume wangu, tutaonana endapo nitarudi nitakieni uzima," amesema.

## Mchekeshaji aaga dunia

MSANII wa ucheshi wa Nigeria, Ada Jesus, amefariki dunia baada ya kusumbuliwa na matatizo ya figo.

Mchekeshaji huyo mwenye miaka 22 amefariki juzi katika hospitali moja jijini Abuja.


Ada alikuwa amelazwa kwa muda wa miezi kadhaa akipatiwa matibabu ya ugonjwa huo ambao uligundulika hivi karibuni.



MAKALA

# Kufikiri na kutumia TEHAMA kulivyomsuka kiuchumi Noreen

Na Mwandishi Wetu



AKILIHUTUBIA bunge juzi jijini Dodoma, Rais Samia Suluhu Hassan, anasema, kwa kiasi kikubwa biashara na shughuli nyingi za uwekezaji na maendeleo duniani zinafanywa kwa njia ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Kwa mujibu wa maelezo yake dunia iko kwenye mapinduzi ya nne ya teknolojia kwa hiyo hakuna mbadala wa TEHAMA ni jambo ambalo halikwepeki ndiyo maana Tanzania haiwezi kukwepa jukumu la kuendeleza miundombinu ya sayansi na teknolojia.

Wakati Rais anayasema hayo wako baadhi ya Watanzania wameshaona fursa hizo za kiteknolojia. Noreen Kira (pichani), ni mmoja wao, anasema fursa za mafanikio ni nyingi kupitia TEHAMA.

Anaziona kuwa fursa za kiuchumi na kiuwekezaji hazihesabiki na kwamba kinachohitajika ni kutumia njia za kisasa ili kuziona, kuzichangamkia na kunufaika nazo.

Akizungumza na Nipashe, hivi karibuni anasema ana miaka 24 na kwamba anamiliki kiwanda cha kuoka keki, mikate pamoja na duka la kuuza bidhaa hizo.

Anasema baada ya kuhitimu katika Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT) mnamo 2019, alianza safari ya mabadiliko ya kisasa ya biashara yao ya familia, akitumia teknolojia.

"Nilichukua biashara hii kutoka kwa mama yangu, ambaye alikuwa na duka karibu na nyumbani kwetu Kiluvya, nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, tangu 2013. Hapo mwanzo, mama alikuwa akiuzia keki na mikate nyumbani na wateja wake walikuwa ni majirani na wapita njia." anasema.

Akiwa mhitimu wa uhandisi wa masuala ya kielektroniki na mawasiliano, alianza kufikiria jinsi ya kutumia maarifa yake na ustadi wa kidijitali kupanua biashara ya familia, ambayo ilikuwa ikifanywa kwa mazoea na kienyeji kwa miaka mingi.

Anakumbusha kuwa alipokuwa mwaka wa pili chuoni hapo, mnamo 2018, alichaguliwa na kampuni ya simu ya Huawei Tanzania kuhudhuria mpango wao wa Uwajibikaji kwa Jamii wa kampuni inaoitwa 'Seeds for the Future', uliokuwa unakusudia kusaidia kukuza vipaji vya vijana kupitia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kuhakikisha kuwa vijana wenye uelewa na wenye kutaka mabadiliko wana ujuzi na fikra zinazohitajika kuwa na ushindani katika maeneo ya kazi ya siku zijazo.

Anaeleza uwa alibahatika kuwa miongoni mwa vijana waliotembelea China katika ziara ya siku kadhaa iliyogharamiwa na kampuni ya simu ya Huawei.

Anasema alipata kushuhudia teknolojia ya hali ya juu pamoja na kupokea mazoezi ya kiufundi katika makao makuu ya Huawei huko Shenzhen, China. Safari hiyo ilimchochea kufikiria kwa ubunifu na kujikita kwenye kutumia teknolojia.

"Nilipokuwa China, nilijifunza somo muhimu kuhusu namna ya kuendesha biashara kupitia miamala ya simu.

Ni vigumu sana kwa watu kubeba fedha nchini China." Anasema na kuongeza kuwa alivyotoka China, Noreen alianza kuhamisha shughuli kadhaa za biashara yake mtandaoni.

Noreen anatumia mitandao ya kijamii kufikia wateja wake. Anatunza rekodi za wateja wake ili kuwarahisishia kuagiza na kupokea bidhaa kwa haraka zaidi. Matokeo yake, huona biashara yake ikibadilika hatua kwa hatua.

**"Nilichukua biashara hii kutoka kwa mama yangu, ambaye alikuwa na duka karibu na nyumbani kwetu Kiluvya, nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, tangu 2013. Hapo mwanzo, mama alikuwa akiuzia keki na mikate nyumbani na wateja wake walikuwa ni majirani na wapita njia." anasema.**

"Zamani, tulikuwa na wateja wachache, lakini kwa sasa, maisha yamebadilika, ninaweza kupata wateja wengi kwa njia za mitandao. Sasa nimeunda mtandao wa wateja, wengine ninawajua na wengine siwajui, ninaweza kuweka picha za kuvutia za bidhaa zangu. Nimejiunga pia na matangazo ya kulipia na inasaidia sana katika kuongeza mauzo haswa wakati wa misimu wa sherehe. Tangu wakati huo biashara yangu imekua haraka sana." anasema.

Noreen hutoa huduma za usambazaji wa keki kwa Dar es Salaam na Pwani na wakati mwingine, anazisambaza zaidi ya mikoa hiyo miwili. Sasa anaweza kuendesha maisha yake na ya familia yake kupitia biashara yake.

Kwa kuwa ujasiriamali wa kidijitali unakua nchini, Noreen anaamini kwa kiwango kikubwa huwa, kuwapa vijana ujuzi huo ni muhimu ili kuongeza ushindani wao katika soko la ajira, kwani ustadi wa dijiti ni moja ya mahitaji ya muhimu ili kupata nafasi.

"Ni muhimu kwa vijana kujiweka sawa katika enzi hii ya kidigitali. Ni wakati wao kupata ujuzi wa kidigiti na kuwa na uwezo zaidi katika soko la ajira au kuweza kuanzisha biashara zao." anashauri.

Kwa jinsi biashara ya mtandaoni inavyoongezeka, Noreen ana mpango wa kufungua maduka mengine Dar es Salaam.

"Ninafurahi sana kuona biashara yangu inakua, lakini kinachonifurahisha zaidi ni kwamba ninaweza pia kuajiri vijana wenzangu na kushiriki uzoefu wangu nao," anasema mhandisi huyo.

# TARI Uyole, yakomboa wakulima wa Mbeya kwa mashine ikaushayo mazao

**Na Eliud Ngondo, Mbeya**

KILIMO ni sekta inayoongoza kuajiri Watanzania wengi, kwa historia ndefu, ikiajiri robo tatu ya umma nchini kupitia uzalishaji mazao ya chakula na biashara.

Unapotajwa Mkoa wa Mbeya, daima unajishughulisha na kilimo kwa asilimia kubwa, hali inayoifanya kubeba wasifu 'Ghala la Taifa la Chakula.'

Maharage yamo katika mazao yanayozalishwa kwa kiwango kikubwa, pia mkoani Songwe, kutokana na hali ya hewa nzuri inayoambatana na mvua za kutosha, kuiwezesha kustawi, huku kukielezwa matumizi yake yanaongezeka maradufu.

Taarifa za soko la maharage katika mikoa hiyo zinaonyesha yanauzwa kwa bei ya kati ya Sh. 28,000 (Sh. 1400 kwa kilo) kwa kilo 20 mpaka Sh. 40,000 (Sh. 2000), kulingana na hali ya uzalishaji katika maeneo tofauti.

Hapo ndipo, baadhi ya wakulima wamekuwa wakichangamkia fursa ya kuzalisha zao hilo na wapo wanaotumia kampuni, vikundi vya wakulima wadogo hata mkulima mmoja, kulingana na uwezo kiuchumi.



Mkurugenzi wa TARI Kituo cha Uyole jijini Mbeya, Dk. Tulole Bucheyeki (kushoto), akimkabidhi Mwenyekiti wa Kikundi cha Walima Maharage cha Upendo, Wilaya ya Mbozi, Daud Bukuku, mashine ya kisasa ya kupigapiga maharage.

### SHIDA INAYOWAKABILI

Kuna baadhi ya matatizo wakulima wanakabiliwa nayo, ambayo wataalamu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzani (TARI) Kituo cha Uyole, Mbeya wanasema walitafiti na kubaini wakulima wanapoteza mazao yao kwa asilimia kati ya 25 na 80, kutoka hatua ya upandaji hadi matunzo.

Mkurugenzi wa TARI Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, anasema wakulima wana nafasi ya kulima vizuri mazao yao, shida iko katika uvunaji na uchakataji, unaosababisha upotevu mkubwa wa mazo hayo.

Anasema, baadhi ya wakulima wamekuwa wakipoteza mazao yao wakati wa kuvuna, kuanika na kuhifadhi na sababu kuu ya upotezaji inaangukia katika matumizi ya zana duni za kilimo.

Dk. Bucheyeki anasema, baadhi ya walima maharage wanapoteza ubora wa zao wakati wa kuvuna, kutokana na kupiga kwa kutumia zana duni zinazopasua maharagwe na kuna sehemu inasababisha zoezi kwa kutokauka vizuri.

Anasema wakulima kupoteza mazao wakati wa mavuno, pia kipindi cha masika kinachombatana na msimu wa mvua muda mrefu, inachangia mavuno hayo yasikauke kwa wakati.

"Mazao mengi wanavuna kipindi cha mvua nyingi na kutokana na teknolojia ndogo ya ukaushaji, wanajikuta sehemu kubwa ya mazao yanaharibika kwa kuoza, wakiwa wameyahifadhi ndani ya nyumba au yakiwa shambani," anasema.

Dk. Bucheyeki anasema, TARI kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Mazao ya Kitropiki (CIAT), wameamua kuwasaidia wakulima zana za kisasa za kupiga na kukaushia maharagwe, ili kupunguza upotevu.

Mkurugenzi huyo anasema mashine hizo mbili, pia mitambo miwili, zina thamani ya Sh. Milioni 11.2, ikilwalenga wakulima waliopo kwenye vikundi.

### MTAFITI ASHAURI

Mtafiti wa Maharagwe kutoka TARI Uyole, Dk. Merry Ndimbo, anasema wanawasaidia wakulima kwa elimu na utoaji mbegu bora zilizofanyiwa utafiti na mashine, ikiwa ni sehemu ya hatua za serikali na wadau kuwasaidia wakulima kiuchumi.

Anasema, amewaunganisha wakulima kuzalisha maharage lishe yenye madini chuma na zinki, huku vikundi pia vinazalisha aina nyingine ili kuongeza ukubwa wa masoko.

"Ili mkulima aweze kufikia lengo lake, anatakiwa kupatiwa huduma iliyokamilika na hii itafikiwa endapo wadau tofauti tutaungana pamoja, kama ilivyofanyika kwenye vikundi hivi ambavyo vinasaidiwa na wadau tofauti, lakini kwa pamoja," anasema Dk.Merry.

### VIKUNDI VYA WAKULIMA

Kikundi cha Upendo kilichopo kijiji cha Senjele, Wilaya ya Mbozi Mkoa wa Songwe, kimepewa mtambo wa kukaushia mazao na mashine ya kupiga piga mazao zaidi ya nane.

Mwenyekiti wake, Daudi Bukuku, anasema mashine hiyo na mtambo wa kukaushia mazao, utawaongezea ubora wa mazao yao tofauti na awali.

Anasema mazao yao kuyakausha kwa kuanika nchini hali inayosababisha mazao kuanuliwa yakiwa na mawe na ndio miongoni mwa kikwazo wanapoenda kuuza bidhaa sokoni.

Bukuku anasema, kwa sasa wana uhakika wa mazao yaliyo safi na salama, kutokana na mtambo huo kufanyakazi ya kukausha na kuyaweka katika hali nzuri, isiyokuwa na mawe.

"Tulikuwa tunalazimika kuajiri watu wengi na kuwalipa pesa nyingi lakini pia zitatusaidia kupunguza upotevu wa mazao yetu," anasema Bukuku.

Kikundi cha wanawake cha Zinduk, kutoka Kata ya Mshewe katika Halmashauri ya Wilaya Mbeya, pia ni mnufaika wa msaada huo.

Mwenyekiti wake, Witness Sikayange, anasema walikianzisha kikundi mwaka 2010 na sasa kina jumla ya wanachama 21, wote wanawake. Walianza kulima ekari 10, lakini mpaka sasa wana ekari 300.

Anasema, walinunua baadhi ya mashamba kutokana na faida ya kilimo hicho, kukiwapo ekari 100 na zingine 200 walizopewa na Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza.

Anasema, awali walitumia mbinu za asili na mbegu za kienyeji, iliyowapa tija ndogo, wakivuna kilo 100 kwa ekari, wakati utafiti wa kitaalamu unaonyesha katika eneo hilo mkulima anatakiwa kupata kilo 800 kwa ekari.

Witness anasema, TARI waliwasaidia kuwapa elimu kuhusu kilimo bora na kuwapatia mbegu za kisasa zilizowapaa matokeo chanya.

"Mpaka sasa tunapanda kilo 30 za mbegu na tunavuna kilo 800 kwa ekari moja na kukiwa na hali ya hewa mbaya tunavuna sio chini ya kilo 600," anasema Sikayange, akifafanua wanalima awamu tatu kwa mwaka, mbili za masika na moja kiangazi

Pia, anasema kikundi hicho kilisaidiwa na taasisi zingine ikiwamo Kilimo Trust na kampuni ya Raphael Group, zilzojengea ghala la kuhifadhi mazao, kabla ya kuyauza.

Anaitaja Raphael Group ni mteja mkuu wa maharage wanayozalisha na imewasaidia mizani ya kidigitali kupima mazao hayo, ili kuachana na iliyopitwa na wakati kibiashara, pamoja na kipima unyevu.

Mama huyo anasema, ni mafanikio ambayo sasa yamezalisha vikundi vingine viwili, kinachojumuisha wazee wa jinsia zote na Jikomboe cha wanaume pekee.

### WAPATIWA MITAMBO

TARI kwa kushirikiana na CIAT, imewasaidia changamoto ukaushaji maharage kwa vikundi hivyo, kila kimoja mtambo mmoja wa kisasa, pia mashine ya kisasa ya kupiga piga maharage baada ya kuvuna.

Mtambo wa kukaushia maharagwe una uwezo wa kukausha mpaka kilo 1,000 kwa siku, ukitumia kati ya saa sita mpaka nane, ukiwa mkombozi wa umma.

Uhusiano wa CIAT, Sylvia Karemera anasema ukaushaji kupitia mitambo hiyo inayotumia jua, unapunguza unyevu hadi chini ya asilimia 15, inaepusha mazao kutoka hasara ya kunyeshewa na mvua au kuliwa na mifugo.

Anasema mbali na kuwasaidia wakulima hao kukausha maharagwe na kupiga piga, pia itakuwa na manufaa ya kukausha mazao mengine kama choroko, mbaazi, mtama, ulezi, uwele, na mahindi.



Mtaalamu wa mitambo ya kisasa ya kukaushia maharagwe kwa kutumia nishati ya jua kutoka katika taasisi ya CIAT, akitoa maelekezo ya kufunga mtambo huo, wakati ikishirikiana na asasi ya TARI Kituo cha Uyole, kukabidhi kwa vikundi vya wakulima vya Zinduka na Upendo, mkoani Mbeya na Songwe. **PICHA ZOTE: ELIUD NGONDO.**

HABARI KIMATAIFA

# Macron ashirki mazishi Idriss Déby

**N'djamena,** CHAD

RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron, amehudhuria ibada ya mazishi ya aliyekuwa rais wa Chad, Idriss Déby, katika mji mkuu wa nchi hiyo N'Djamena na kuzikwa katika mkoa wake jana.

Deby aliuawa Jumatatu, wiki hii katika eneo la mapigano dhidi ya wapiganaji wa Front for Change and Concord in Chad (Fact), kikundi cha wanajeshi waasi kilichoundwa na maafisa wa kijeshi mwaka 2016.

Macron aliwasili kuelekea mjini N'Djamena licha ya onyo kutoka kwa waasi kwamba, kiongozi huyo wa kigeni hapaswi kuhudhuria kwa sababu za kiusalama.

Viongozi wengine waliohudhuria ni kutoka mataifa ya Mali na Guinea.

Baada ya kutolewa kwa heshima za kijeshi na hotuba mbaliambali, sala ilifanyika katika msikiti wa Grand Mosque uliopo N'Djamena.

Baadaye mwili wa Déby ulisafirishwa kwa ndege hadi Amdjarass, kijiji kidogo kilichopo karibu na mji anakotoka wa Berdoba, uliopo zaidi ya kilomita 1000 kutoka mji mkuu, karibu na mpaka wa Sudan.

Rais Déby alikuwa mtu muhimu katika mkakati wa usalama katika kanda ya Sahel.



Maofisa wa ngazi ya juu kutoka jeshi la Chad, wakibeba jeneza la aliyekuwa Rais wan chi hiyo Idiss Deby kwa ajili ya ibada ya kuaga mwili katika mji wa N'Djamena jana. (**PICHA: AFP**)

Baraza la kijeshi linaloongozwa na mwanae, Jeneral Mahamat Idriss lilichukua madaraka baada ya kifo chake anaungwa mkono kwa kiasi kidogo na jeshi, ingawa anaungwa mkono na mtawala wa Ufaransa.

Jenerali Déby, 37, alisema jeshi litafanya uchaguzi wa kidemokrasia katika kipindi cha miezi 18 ijayo, viongozi wa upinzani wamelaani hatua yake ya kuchukua mamlaka na kuitaja kama mapinduzi na jenerali wa kijeshi, maafisa wengi wanapinga uongozi wake wa mpito.

Ni mpango ambao pia waasi waliupinga huku pia wakionya kuwa watasitisha kipindi kidogo kilichokuwepo cha usitishaji mpigano.

Mgawanyiko ndani ya jeshi na upinzani vinamaanisha kuwepo kwa ukosefu mkubwa wa usalama huku kukiwa piwa nma changamoto za kiuchumi, wakati Chad inaingia katika kipindi cha mpito.

**BBC**

## Madaktari washauri Navalny kusitisha mgomo wa kula

**Moscow,** URUSI

MADAKTARI binafsi wa mwanasiasa wa upinzani na mkosoaji mkubwa wa serikali ya Urusi, Alexei Navalny, wamemtaka kiongozi huyo kusitisha mgomo wa kutokula chakula haraka iwezekanavyo, ili kunusuru afya na maisha yake.

Katika ujumbe wake uliojaa hisia, Navalny alisema juzi kupitia ukurasa wa Instagram kwamba anajisikia fahari na mwenye matumaini.

Siku ya Jumatano maelfu ya wananchi waliandamana mitaani kote nchini Urusi, baada ya nchi za magharibi kuionya Kremlin juu ya athari zitakazojitokeza endapo mwanasiasa huyo atafia mikononi mwao.

Zaidi ya watu 1,900 walikamatwa wakati wa maandamano hayo.

Kuanzia Machi 31, mwaka huu, mwanasiasa huyo anayetumikia kifungo alitangaza kuanza mgomo wa kutokula akidai kupatiwa matibabu sahihi.

Mamlaka za Urusi, zilimuhamishia katika hospitali binafsi siku ya Jumanne kwa matibabu zaidi.

**DW**

## Biden afungua mkutano tabianchi

**Washington,** MAREKANI

RAIS Joe Biden, ameahidi kupunguza kwa nusu viwango vya utoaji wa gesi ya ukaa nchini Marekani, kufikia mwishoni mwa muongo huu, akifungua mkutano wa kilele wa mtandaoni uliohudhuriwa na viongozi 40 wa dunia kuhusu mabadiliko ya tabianchi.

Mkutano huo wa siku mbili unalenga kuyahamasisha mataifa yenye uchumi mkubwa kuweka malengo zaidi ya kupunguza viwango vya gesi ya kaboni

Inatazamwa kuwa mkutano muhimu kwa maandalizi kuelekea mkutano wa mazingira wa Umoja wa Mataifa (UN), utakaofanyika mjini Glasgow, Scotland, mwezi Novemba.

Katika siku za kwanza ofisini, Biden alitangaza mpango mpya wa mazingira, wa jinsi Marekani itakavyoshirikiana na Benki ya Dunia (WB) na Shirika la Fedha Duniani (IMF), kuzisaidia nchi maskini kupunguza utoaji wa gesi chafu kwa ajili ya kuyalinda mazingira.

**DW**

## Bobi Wine kulipa mamilioni kukomboa gari lake kifahari

**Kampala,** UGANDA

MAMLAKA ya Mapato Uganda (URA), imemtaka kiongozi wa upinzani na mgombea wa uchaguzi Robert Kyagulanyi, al maarufu Bobi Wine, kulipa ushuru ya shillingi za Uganda milioni 337 sawa na dola 166,700, ili arudishiwe gari lake la land Cruiser.

Taarifa ya uamuzi huo kwa kiongozi wachama cha National Unity Platform (NUP), inakamilisha mchakato wa mamlaka ya forodha nchini humo kutathmini thamani ya gari hilo linalozuia risasi.

Gari hilo awali lililipiwa ushuru mdogo kwa kulinganishwa na gari lingine la kawaida.

Akijibu juu ya hatua kuthamanishwa upya kwa gari lake kupitia ujumbe wake wa twitter, Bobi Wine alilalamikia hatua hiyo.

''Baada ya majaribio kadhaadhidi ya maisha yangu, baadhi ya marafiki zangu walinipatia gali linalozuia risasi. Mara ya kwanza mambo yote alikuwa mazuri kwasababu halikwa kwa jina langu.



"Interpol, Idara ya uchunguzi ya polisi na URA wote walilichunguza na kuliidhinisha.

"Ushuru unaotozwa na URA tuliilipa. Mambo yalianza kugeuka wakati walipogundua kuwa ni gari langu'' alisema Wine.

**BBC**

## Urusi yaondoa wanajeshi mpaka wa Ukraine

**Moscow,** URUSI

Urusi imeanza kuwaondoa wanajeshi wake ambao wamekuwa wakifanya mazoezi ya kivita karibu na mipaka jirani yake Ukraine. Taarifa iliyotolewa na wizara ya Ulinzi ya nchi hiyo, ilisema misafara ya wanajeshi wa nchi hiyo tayari inaelekea kwenye vituo vya treni, viwanja vya ndege pamoja na bandari kwa matayarisho ya kuondoka kuanzia jana.

Waziri wa Ulinzi Sergei Shoigu, alisema mazoezi ya kijeshi yaliyokuwa yakifanyika yamemalizika na wanajeshi wote watakuwa wamerejea kambini ifikapo mwanzoni mwa mwezi Mei. Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, aliikaribisha hatua hiyo, lakini alilisisitiza kuwa jeshi la nchi yake litasalia imara baada ya mvutano wa wiki za hivi karibuni kufuatia hatua ya Urusi ya kuongeza idadi ya wanajeshi wake karibu na mipaka ya nchi hiyo

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa**
**Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KAHAMA IMPORT AND EXPORT** Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC. 938 AYK.** yenye Chassis no. **LTZPCJLN4F6200614**, Engine no. **156FMIF0003344.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake. Taarifa ya Polisi. **KAH/TR/RB/165/2021.**

---

**JAMHURI YA MUUNGNO WA TANZANIA**
**KATIKA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**LA MWANZA**
**MAOMBI NAMBA 464 / 2020**
**BALTAZARI KALANGI………………..MWOMBAJI**
**DHIDI YA**

1. NZULA MATHIAS
2. MAFURU B. MAFURU
3. BURABO JOSEPH
4. HUSSEIN JOSEPH
5. KASISI JOSEPH
6. SHABAN JOSEPH
7. ABUBAKALI JOSEPH
8. TABU JOSEPH
9. DOAS CHARLES

……………….WAJIBU MAOMBI

**TAARIFA YA KUTAJWA KWA SHAURI**
**POPOTE MLIPO WAJIBU MAOMBI HAPO JUU**

BALTAZARI KALANGI, amefungua Shauri la maombi mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba la wilaya ya Mwanza ambalo limepangwa kutajwa mnamo tarehe 29/04/2021. Hivyo basi mnatakiwa kuleta utetezi wenu mnamo au kabla ya tarehe ya kutajwa. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika masijala ya wazi ya Baraza hilo.

Endapo hamtatekeleza hayo, shauri litasikilizwa upande mmoja na maamuzi kutolewa.

Imetolewa na kutiliwa saini / muhuri wa Baraza leo tarehe 26 mwezi 02 mwaka 2021.

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**MWANZA**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJ

TWININGEGE ATUPELE MLUNGU ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJ AINA YA TVS KING YENYE NAMBA ZA USAJIL MC 758 BWX RANGI YA KIJANI.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI MBE/MBE/RB/210843/2021

---

## NOTISI YA KULIPA DENI

**TUJIJENGE TANZANIA LIMITED,** inatoa notisi ya siku sitini (60) kwa Ndugu EMMANUEL JOHN NDULU (Mdaiwa Sugu) unakumbushwa kulipa deni lako la mkopo unaodaiwa bila kukosa tangu siku ya tangazo la notisi hii.
Kushindwa kulipa taratibu zingine za urejeshwaji wa deni lako la mkopo zitafuatwa.

**Kwa mawasiliano na malipo fika ofisi zilizopo Kijitonyama-Makumbusho- Makao Makuu Au piga namba +255 (022) 2774742/3**

---

## NOTISI YA KULIPA DENI

Kampuni ya **CHAMPION AUCTION MART** kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD** tunatoa notisi ya madai ya muda wa siku kumi na nne(14) kwa wadaiwa waliopo kwenye tangazo hili, wawe wamelipa madeni yao wanayodaiwa na taasisi ya Tujijenge Tanzania Ltd tangu siku ya tangazo hili gazetini.

1. ALOYCE JOHN MNYARI–MTAA WA MPIJI MAGOE, KATA YA MBEZI
2. BERNARD DAUD NKEYEMBA – MTAA WA KINZUDI, KATA YA GOBA

**MASHARTI**
Kushindwa kulipa kwa wakati tutalazimika kuchukua hatua zaidi za kisheria ikiwa ni pamoja na kutangaza uuzwaji wa dhamana za mkopo kwa njia ya mnada.

**Mawasiliano piga: 065300503/0629464764**

---

**IN DISTRICT COURT OF GEITA**
**AT GEITA**
**CASE NO 3 OF 2021**
**GEITA DISTRICT COUNCIL PLANTIFF**
**VERSES**
**SILVESTER MALALE IKANGALA**
**DEFENDANT**

**NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION**
**TAKE NOTICE THAT**, the above case fixed for mention on the 27th day of April 2021 at 8.30am in the afternoon.
**YOU ARE** required to appear in this court without fail and you must produce on that day all the documents which intend to rely in support of your case.
**GIVEN UNDER** my hand and the **SEAL** of the Court this 22nd day of **APRIL**

**By; SENIOR RESDENT MAGISTRATE**
**GEITA**
**TO BE SERVED UPON:**
**SILVESTER MALALLE IKANGALA OF BUSANDA**
**0624269874**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TUNDU A.M. LISSU** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 639 BSW LAND ROVER DISCOVERY.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **WMB/RB/241/2021.**

---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI**
**MWANZA**
**SHAURI LA MAOMBI NA. 141 YA 2020**
**(Asiria shauri la Madai Na 80 / 2019)**
**AUDAX FAIDAKIBALA……..MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**YUNNUS YAMA ADAM…………MJIBU MAOMBI**
**KWA: MDAIWA**
**POPOTE ULIPO**

Mahakama hii inawafahamisha kwamba mdai ameleta maombi yake dhidi yenu.
Nakala yake inapatikana katika Mahakama hii.
Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 11/05/2021 saa 2:30 asubuhi na unatakiwa kuwepo, au kuwakilishwa kisheria pamoja na kuleta utetezi wako dhidi ya maombi hayo ya kukaza Hukumu.
Zingatia kwamba kutofika kwako tarehe hiyo, shauri litaanza kusikilizwa bila ya wewe kutaarifiwa tena, na maamuzi kutolewa.
Imetolewa kwa mkono wangu na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe **21/04/2021**

**HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI MFAWIDHI**
**MWANZA**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RAMADHANI SHABANI SEIF** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 618 DDS – TATA**. Chassis namba **MAT382042F7R01280.** Engine namba **497TC93AUY803179**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DSM/PHQ/RB/206598/2021.**

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MWANZONI ilionekana ni fahari. Wazazi kupata mtoto wa kike. Akaja kuwa msichana mzuri aliyeumbwa akaumbika na kutamaniwa na kila mtu, ni sifa kubwa. Wakati mwingine mzazi hupata hata vizawadi vidogo kutoka kwa watu mbalimbali bila kujua kuwa nia ni kutengeneza mazingira kwa binti yao. Kinyume chake mzee Ngoma na mkewe Fatuma wanapata mtoto wa kike Bishada ambaye anaondokea kuwa tishio kwenye kijiji cha Mtakuja kwa urembo wake.

Badala ya kuwa tija na faraha kwa wazazi wake anageuka kuwa balaa. Wazazi wanakuwa hawana amani kutokana na vitisho mbalimbali ikiwemo kuuawa kutoka kwa watu mbalimbali ndani na nje ya kijiji hicho. Inakuwa tafrani. Kijiji hakikaliki. watu wanatafutana. Moto unawaka. Bishada mwenyewe maisha yake yanakuwa hatarini. Fuatilia kisa hiki ambacho kitakuacha mdomo wazi.

# Aolewe au afe-**3**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

"Enhee bora nimekuona. We Bishada kwa nini umenitia aibu mimi na ndugu zangu, umekataa mimi nisikuoe?"

"Uliniambia kama wewe unaleta barua kwetu?" Bishada alijibu.

"Siyo lazima, mimi nilikuona siku moja ukiwa na shoga zako, nikatokea kukupenda, nikauliza jina na unakoishi wakaelekezwa ndiyo nikaleta barua kwenu."

"Utaletaje barua kwetu kabla ya kuiona mimi kwanza, halafu ndiyo nikakwambia lete au usilete?"

"Kwa hiyo hilo ndiyo kosa langu?"

"Ndiyo, labda mimi nina mchumba mwingine je?"

"Kwa hiyo nianze upya? Mimi nimekupenda nilete barua kwenu?"

"Si umeleta umekataliwa. We hujui kukataliwa?"

"Sasa Bishada, mimi mwenzako nimekufa kwako, nakupenda sana wewe."

"Sikatai kwamba unanipenda na siyo wewe tu. Wengi wananipenda na wameleta barua nyumbani, lakini mimi sitaki. Sijaamua kuolewa." Bishada alimkatisha tamaa Duma.

Hakuwa na la kuongea. Alionekana kuwa na mawazo, hasira, vyote vikichanganyikana na aibu.

"Haya, poa tu, lakini ipo siku tu."

"Lo, umechelewa babu." Bishada alijibu kwa nyodo.

Ukweli ni kwamba Bishada hakuwa na mchumba yoyote. Hakuwa na mpenzi yoyote. Bado aliamini kuwa ana nafasi ya kutulia kuliko kufanya papara ya kuolewa.

Njiani alikutana na kijana mwingine anaitwa Mtoka. Yeye pia alikuwa ni mmoja wa walioleta barua hivi karibuni na kupigwa chini.

"Kumbe Bishada umenitakalia mimi, halafu unamkubali Duma. Wewe mtoto wa kijiji cha pili atakusaidia nini badala ya kutukubali sisi wa kijiji hiki hiki?"


"Hivi wewe una akili kweli?" Alimuuliza kwa hasira.

"Akili ya nini wakati mimi nimekuona laivu pale kisimani mkiongea?"

"We ulisikia tulikuwa tunaongea nini?"

"Alete barua kwenu."

"Haya ndiyo nimekwambia alete barua kwenu anioe, wewe unasemaje?" Bishada aliamua kusema hivyo.




"Yaani mimi ndiyo umenikataa umemkubali Duma kweli?"

"Ndiyo?"

"Nitahakikisha hakuoi."

"Kwani wewe ndiyo nani? Baba yangu, mama au mjomba?"

Mtoka hakujibu kitu. Bishada akiwa na ndoo yake kichwani alimuacha amesimama, akaanza kupiga hatua za madaha moja baada ya nyingine kuwahi nyumbani.

Ilimshangaza kuona yeye kukataa kuolewa imekuwa kama deni. Kila mtu anamlaumu. Wazazi wanalaumu. Waposaji wanalaumu na kulalamika. "Mimi mwenyewe sitaki. Kwani si mpaka mimi nikubali. Kuolewa bila mimi kutaka unahusu?" Alijikuta akiongea mwenyewe wakati akitua ndoo yake maji baada ya kufika nyumbani.

************************************

"Nilikuwa nakutafuta siku zote hizi we mwanakharamu. Kwa nini umetoka kijiji chenu huko kuja huku kutaka mchumba. Kwani kwenu hakuna wanawake?"

"Kwani imekatazwa kwenye kijiji chenu kuja kuchumbia?"

Zilikuwa ni sauti za wanaume wawili. Mtoka na Duma. Mtoka ni mwanakijiji cha Mtakuja ambacho ndicho kina msichana Bishada. Msichana anayesumbua wanaume wa vijiji vyote jirani, wakipigana vikumbo kumtongoza, wengine kutaka kumuoa kabisa. Lakini ngoma bado ni ngumu. Mwenye hakubali.

Sasa imesababisha watu kuanza kugombana wenyewe kwa wenyewe.

"Nyinyi ndiyo mtaotuzibia riziki. Kwa nini huko kwenu wasichana hakuna, au wote si warembo?" Mtoka alimuuliza Duma kwa namna ya kejeli.

"Huku nako kuna wanaume wa kuoa. Wanaume wenyewe wote walevi nyinyi, mnaweza kummiliki mtoto kama Bishada?" Duma naye alijibu kwa nyodo.

"Maana siku hizi kwenye kijiji chenu cha Ilembo hukai, kiguu na njia huku, Bishada si alishakukataa wewe?"

"Nani kakataa? Mimi ndiyo mumewe mtarajiwa."

Maneno hayo yalimuumiza sana Mtoka. Kwa sababu alikuwa ameshapeleka posa yake na kukataliwa, alijua fika huenda ni kweli Duma amekubaliwa kweli.

"Yaani mimi ndiyo umenikataa umemkubali Duma kweli?"

"Ndiyo?"

"Nitahakikisha hakuoi."

"Kwani wewe ndiyo nani? Baba yangu, mama au mjomba?"

Aliyakumbuka maneno aliyokuwa akiongea na Bishada siku tatu zilizopita njiani wakati akitoka kisimani.

Hasira zikampanda Mtoka.

"We Boya tu, huwezi kumuoa Biashada." Duma alizidi kumuumiza roho mwenzake. Naye alijua kabisa kuwa barua yake ya posa ilidunda. Lakini bado hakukata tamaa ya kumfukuzia kimwana huyo.

Wakati akijua labda Mtoka atajibu kwa maneno, alijibu kwa vitendo. Teke moja la mbavu lilimpata na kumsababishia maumivu makali. Alipepesuka, lakini hakukubali. Alipiga hatua tatu mbele na kumrukia.

Mtoka alijua hilo. Alikua tayari kukabiliana na chochote kile. Wanaume hao wakawa wameshikana kama wacheza mieleka na kusukumana, kila mmoja akitaka kumuangusha mwenzake chini.

Walipepesuka na kuanguka wote. Walianza kubimbirishana. Kila mmoja alijitahidi kutaka kumshinda mwenzake.

Wakati wakiendelea na ngumi zao zilizokuwa na staili yoyote na za kutumia zaidi nguvu kuliko akili, walijikuta wakicharazwa bakora zilizowapata mwilini kisawasawa.

Baada ya kuona ngumi hizo, baadhi ya watu hasa wenye umri mkubwa waliamua kuwaachanisha kwa staili hiyo ya kukata fimbo na kuwacharaza. Huo ndiyo ukawa mwisho wa ngumi hizo zilizotokana na wivu.

**Nilikuwa nakutafuta siku zote hizi we mwanakharamu. Kwa nini umetoka kijiji chenu huko kuja huku kutaka mchumba. Kwani kwenu hakuna wanawake?**

**********************************

"Mwanangu hadi naogopa mama yako."

"Unaogopa nini mama?"

"Nimesikia jana yule kijana wa mzee Mitimingi, anaitwa Mtoka, kapigana na kijana mmoja kutoka Kijiji cha Ilembo kwa ajili yako."

"Kwa ajili yangu?" Biashada aliuliza.

"Ndiyo. Nimekuja kupewa taarifa leo asubuhi hapa, kuwa jana kulikuwa na timbwili njia ya kwenda mauzoni. Watu wamepigana, kisa binti yako Biashada. Mimi nikawauliza kafanyaje? Wakaniambia wanamgombea? Ukweli hata mimi sikuelewa, wanapigania nini wakati wote walileta barua na zimekataliwa?"

Bishada ambaye alikuwa anamsaidia mama yake kuchambua mchicha, alitabasamu. Ni tabasamu ambalo lilikuwa dhahiri machoni mwa mama yake Bi.Fatuma.

"Kumbe unaujua huo ugomvi?"

"Niujue wapi. Ila nilihisi kama utatokea hivi."

"Kwa nini?"

"Kuna siku nilikuwa kisimani, akafika kijana mmoja anaitwa Duma. Yule ambaye alikuwa wa kwanza kuleta barua hapa. Akaniuliza kwa nini umeikataa barua yangu. Nikamwambia siyo lazima na mwanaume siyo wewe peke yako. Kwani wewe ndiyo una sifa za kuoa tu wengine hawana? Halafu nikamwambia siku nyingine akitaka kuoa kwanza ni vizuri awe anawasiliana na kuolewaji, vinginevyo atakuwa anakosa wachumba kila siku. Wachumba wa sasa siyo kama wa zamani ambao barua zinakuja tu, lakini hawamjui ni nani."

"We mtoto wewe. Una maneno siku hizi."

ITANEDELEA JUMAMOSI




# KOEMAN AELEZA MKAKATI WA UBINGWA

**BARCELONA,** Hispania

ROALD Koeman amesema kikosi chake kitapambana hadi mechi ya mwisho kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Barca Alhamisi usiku waliwafumua Getafe mabao 5-2 kwenye mchezo wa LaLiga uliopigwa katika dimba la Camp Nou.

Barcelona sasa wapo katika nafasi ya tatu, pointi moja juu ya Sevilla na pointi mbili nyuma ya Real Madrid, na tano nyuma ya Atletico Madrid.

Barcelona wakiwa na mchezo mmoja mkononi, wanawinda kwa hali na mali kila pointi inayoweza kupatikana, kwa ajili ya kujihakikishia wanabeba taji hilo la Ligi Kuu.

Baada ya ushindi huo, Koeman amesisitiza kuwa anaamini kuwa wamepata matokeo mazuri, kwa sababu walijikita kwenye kutafuta na kutumia nafasi vizuri.

Kwa mujibu wa Koeman, Barcelona si timu bora zaidi ukilinganisha na zingine tatu (Real Madrid, Atletico Madrid na Sevilla) kwa sababu nazo zinafanya vizuri. Lakini wanataraji kupambana vilivyo hadi mechi ya mwisho.



# *Perez bado akomaa na Super League*

**MADRIDR,** Hispania

RAIS wa Klabu ya Real Madrid, Florentino Perez, ambaye pia alitajwa kuwa Mwenyekiti wa Ligi mpya ya Ulaya (European Super League), amesema madai ya ligi hiyo itaua ligi za ndani ya nchi si ya kweli.

Perez amesema kuwa ligi hiyo haijafutwa bali imesimama kwa muda kutokana na timu sita ambazo zinashiriki Ligi Kuu England (EPL) kujitoa, ingawa awali zilikubali kushiriki ambazo ni Chelsea, Liverpool, Arsenal, Manchester United, Tottenham Hotspurs na Manchester City.

Ligi hiyo ambayo ilitangazwa itaanza hivi karibuni, imekuwa ikipingiwa na wadau mbalimbali wa soka pamoja na mashabiki, ambapo wameweka wazi ya kuwa itavuruga utamu wa EPL pamoja na mashindano mengine.

Lakini Perez anaamini kwamba, inawezekana wamekosea katika kuuelezea mradi huu.

"Nasikitishwa na hiki kinachoendelea, tumekuwa tukiufanyia kazi mradi huu kwa miaka mitatu sasa," alisema Perez akinukuliwa na Marca.

Akiongezea: "Katika timu 12 anzilishi msimu uliopita, tulipata hasara ya euro milioni 650. Ila msimu huu inaweza kuwa mara mbili au tatu ya hiyo."

# Lingard na mkasa wa corona kumstaafisha soka

**LONDON,** England

NYOTA wa Manchester United anayecheza West Ham United kwa mkopo, Jesse Lingard, ameelezea namna ambavyo mlipuko wa virusi vya corona ulivyokuwa mgumu kwake mwanzoni mwa msimu huu, kiasi cha kutamani kuacha kucheza soka.

Akizungumza na kipindi maalum cha Youtube, Lingard alielezea jinsi miezi kadhaa iliyopita ilivyokuwa migumu kwake kwenye mchezo huo.


Lingard ambaye hakuwa na namba kule United na hivyo kupelekwa kwa mkopo West Ham, kwa sasa anaonekana kuwa kwenye kiwango cha kuvutia dimbani.

Baada ya kujiunga na West Ham kwa mkopo katika dirisha dogo la usajili la Januari, Linagrd amekuwa katika kiwango bora zaidi.

Amecheza mechi 10 na kufunga mabao tisa huku akitoa pasi za mabao manne, na sasa akitajwa kuhitajika na klabu kadhaa England na Ulaya.

"Kipindi kile nilijihisi kwamba mimi sio Jesse Lingard... hata nikiwa uwanjani nilitamani nitoke tu... sikutaka kuwapo pale," alieleza Lingard.

"Niliendа uwanjani na nilifurahi kukaa benchi, na wala sikuwa mimi... Ningeweza kuacha soka kwa urahisi sana kipindi cha 'Lockdown', lakini nilipata msaada wa madaktari ambao walinishauri kisaikolojia na kunirudisha mchezoni."



# Zlatan: Nitabakia AC Milan maisha yote

**MILAN,** Italia

STRAIKA wa AC Milan, Zlatan Ibrahimovic, amesherekea kusaini mkataba mpya kwa kusema kuwa kwa namna anavyojihisi kuwa klabuni hapo, anaweza kubakia hapo maisha yake yote.

Nyota huyu mwenye umri wa miaka 39, amesaini mkataba wa mwaka mmoja zaidi ambao unamfanya aendelee kuwapo klabuni hapo hadi anapofikisha umri wa miaka 40.

Mara baada ya kusaini mkataba huo, Ibrahimovich amesema Milan kwake ni kama nyumbani, na atafurahia kuendelea kuwapo klabuni hapo kwa muda mrefu zaidi.

"Ninafuraha sana, niliisubiri siku hii na sasa nina mwaka mmoja zaidi, kitu ambacho ni muhimu zaidi kwangu," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Kama nilivyosema wakati wote, kuichezea Milan kwangu ni kama kuwapo nyumbani, nahisi furaha sana, ninaipenda klabu kwa jinsi inavyonifanya nihisi, watu wote wanaofanya kazi hapa, wachezaji wenzangu, kocha na mashabiki wananifanya niwe na furaha wakati wote."

Nyota huyo wa kimataifa wa Sweden, anaamini kuwa Stefano Pioli ni kocha sahihi, mwenye uwezo wa kufanya makubwa katika kikosi cha Milan, na anatarajia atapiga hatua kubwa klabuni hapo.





# MADRID, BAYERN KWA CAMAVINGA

**MUNICH,** Ujerumani

BAYERN Munich imeungana na Real Madrid katika mbio za kuwania saini ya mchezaji wa Rennes, Eduardo Camavinga, katika jitihada za kuboresha eneo la kiungo la timu hiyo.

Camavinga anayecheza nafasi ya kiungo ya timu ya Rennes ana umri wa miaka 18, lakini ukomavu wake kwenye soka umemfanya kuwekwa kwenye rada za mabingwa LaLiga, Madrid na sasa mabingwa wa Ujerumani, Bayern wanahitaji huduma yake.

Bayern wanatafuta mrithi wa Joshua Kimmich na Leon Goretzka ambao wanatajwa kwamba wanataka kuondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu.

Awali, walihitaji kumchukua Florian Neuhaus wa Borussia Monchengladbach, lakini dau la pauni milioni 39 waliloweka Gladbach limewakatisha tamaa. Benchi la ufundi la Bayern limeahidi kumpa Camavinga muda wa kutosha kuchezea timu hiyo kwani wanatambua ubora wake.

Camavinga atakuwa ni mchezaji wa tisa wa Ufaransa kuichezea Bayern Munich kama uhamisho wake utakamilika. Bayern kwa sasa bado haijatangaza mrithi wa kocha wao, Hans Flick, ambaye ametangaza kwamba, anaondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu.

Hata hivyo, taarifa zinadai kwamba, Flick anakwenda kuchukua mikoba ya timu ya Taifa ya Ujerumani kutoka kwa Joachim Low ambaye anamaliza muda wake baada ya michuano ya euro 2020 inayofanyika Juni mwaka huu.

# *Erik Lamela kurudi AS Roma*

**LONDON,** England

WINGA wa Tottenham Hotspur, Erik Lamela, anatarajiwa kuondoka katika timu hiyo punde mkataba wake wa sasa utakapofikia mwisho, kwa mujibu AreaNapoli.it.


Kwa mujibu wa ripoti, Lamela anaweza kurejea nchini Italia, katika klabu yake ya zamani ya AS Roma ambapo aliichezea kabla ya kuhamia Tottenham.

"Lamela yuko tayari kuondoka Tottenham, na uhamisho wa Serie A ukionekana kama hatua inayowezekana," iliripoti AreaNapoli.it.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, alijiunga na Spurs kutoka Roma mwaka 2013, lakini hakuwahi kuishi sawa kama mbadala wa Gareth Bale.

Lamela hadi sasa ameshindwa kucheza michezo 20 ya ligi tangu msimu wa 2015-16.

Awali, Lalema aliripotiwa kwamba anawaniwa na Napoli, lakini klabu hiyo imeachana na mpango wa kumsajili raia huyo wa Argentina, hivyo ana nafasi ya kwenda kule Roma.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI AJIWEKEA TENA REKODI NYINGINE ULAYA

Sasa aungana na Ronaldo kuwa wachezaji pekee katika ligi tano kubwa Ulaya ambao wameweza...

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi amefikisha mabao 25 katika Ligi Kuu Hispania, LaLiga, msimu huu wakati Barcelona ikishinda 5-2 dhidi ya Getafe pale Camp Nou, Alhamisi usiku.

Nahodha huyo wa 'Blaugrana' hao alifunga mabao mawili na kufikisha idadi hiyo na hiyo ilimaanisha yeye na Cristiano Ronaldo, ndio wachezaji pekee kutoka ligi tano kubwa za Ulaya kufikisha mabao 25 au zaidi katika misimu 12 mfululizo.

**Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, yupo tofauti kidogo na Ronaldo kwani yeye ameweza kufikisha rekodi hiyo kwa misimu 12 mfululizo kuanzia msimu wa 2009-2010 katika klabu moja.**

Wakati Ronaldo amefikisha idadi ya mabao 25 akiwa katika klabu tofauti, ya Manchester United, Real Madrid na klabu yake ya sasa Juventus, ambako tayari amefunga mabao 25.

Mabao hayo mawili pia yalimaliza ukame kwa Messi kwenye michezo ya ligi ya nyumbani dhidi ya Getafe.

Messi hapo awali hakuwa amewahi kufunga katika mechi zake tatu za hivi karibuni dhidi ya timu hiyo kwenye Uwanja wa Camp Nou.

Na hiyo ilikuwa ni rekodi yake ndefu zaidi ya kutofunga nyumbani dhidi ya Getafe kwenye mashindano ya nyumbani.

## ZISIKUPITE

### UNITED BADO KWA SANCHO

MATUMAINI ya Manchester United kumsajili mshambuliaji wa England, Jadon Sancho, 21, kutoka Borussia Dortmund, huenda yamepata nguvu mpya kutokana na taarifa kwamba Makamu Mwenyekiti Mtendaji wao, Ed Woodward anatarajiwa kuondoka klabuni hapo. ***(Star)***

### CAKIR AWANIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL huenda ikamkosa Ugurcan Cakir, 25, ambaye wamekuwa wakimnyatia kwa muda mrefu. ***(Fotospor, via Team Talk)***

### JUVE KUMTOA RABIOT

JUVENTUS itakuwa tayari kumtoa kiungo wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot, 26, kwa Manchester United kama sehemu ya mpango wa kumpata mlinzi wa Brazil, Alex Telles, 28. ***(Calciomercato)***

### CAVANI KUONDOKA UNITED

MSHAMBULIAJI wa Uruguay, Edinson Cavani, 34, amekutana na maofisa wa Manchester United na kusisitiza azma yake ya kutaka kuondoka klabuni hapo na kurejea Amerika Kusini kuwa karibu na familia yake. Katika miezi ya hivi karibuni Cavani amehusishwa na uhamisho wa kwenda Boca Juniors. ***(Depo)***

### SMITH HAMTAKI BARKLEY

KOCHA Dean Smith, amesema Aston Villa haina mpango wa kumsajili kiungo wa kati wa Chelsea na England, Ross Barkley, 27, kwa mkataba wa kudumu wakati ule wa mkopo utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu. ***(Mirror)***

### ROMA WAMTAKA VESTERGAARD

AS Roma wanajiandaa kukutana na wawakilishi wa Jannik Vestergaard, 28, wanaposhughulikia mpango wa kumsajili mlinzi huyo wa Southampton ambaye pia anasakwa na Tottenham na Juventus.***(Tuttomercatoweb)***

### LAMELA KUACHANA NA SPURS

WINGA wa Tottenham Hotspur, Erik Lamela, 29, yuko tayari kuondoka klabuni hapo na kurejea Italia. ***(Area Napoli, via Team Talk)***

### AARONS AWANIWA ULAYA

WEST Ham imeungana na Barcelona, Bayern Munich na Tottenham Hotspur katika kinyang'anyiro cha kumsaka beki wa Norwich City na England, Max Aarons, 20, huku klabu hiyo ya Ligi Kuu England ikitaja dau lake kuwa ni pauni milioni 30. ***(Independent)***

### BURNLEY WAMTAKA BENTALEB

KLABU ya Burnley inataka kumsajili kiungo wa kati wa Algeria, Nabil Bentaleb, 26, kutoka Schalke msimu huu wa kipindi cha majira ya joto, wakati mkataba wake utakapofikia mwishoni. ***(Sun)***

### RASPADORI LULU INETR, JUVE

KLABU ya Sassuolo wametangaza kumuuza kwa pauni milioni 13, mshambuliaji wa Italia, Giacomo Raspadori, 21, ambaye amehusishwa na uamisho wa kwenda Inter Milan na Juventus. ***(Calciomercato)***

## Straika Simba Queens, Alliance vita vya kiatu

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALI wawili wanaookimbizana katika mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara, mshambuliaji wa Simba, Oppah Clement na straika wa Alliance Girls, Aisha Juma, watakuwa na nafasi ya kuongeza wigo wa mabao endapo makocha wao watawapanga wakati timu zao zitakaposhuka dimbani leo.

Alliance itakuwa mwenyeji wa Simba Queens leo katika Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza wakati huu timu hizo zikirejea dimbani kwa mara ya kwanza baada ya ligi hiyo kusimama kwa muda kupisha maombolezo ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli.

Hadi sasa Oppah wa Simba Queens ndiye anayeongoza orodha ya wafungaji bora katika ligi hiyo akiwa na mabao 23 akifuatiwa na Aisha wa Alliance Girls ambaye amecheka na nyavu mara 21.

Straika anayewafukuzia kwa karibu, Fatuma Mustafa wa JKT Queens yeye alikuwa na mabao 20 kabla ya mechi yao ya jana dhidi ya Kigoma Sisterz.

## Yanga, Tambwe wamalizana deni

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imemalizana na aliyekuwa straika wake, Amissi Tambwe, kwa kumlipa deni lake kiasi cha Sh. milioni 52 ambazo zilikuwa ni mishahara ya miezi miwili pamoja na baadhi ya pesa zake za usajili.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema tayari wameshamlipa pesa zake zote zikiwamo gharama za mawakili, hivyo sasa wapo huru.

"Tumeshamalizana na Tambwe na sasa tunaangalia mengine tena. Unajua si rahisi kudhibiti hali hii kwa sababu kuna madeni mengi ya zamani kabla ya uongozi huu kuingia, hata deni hili lilikuwa la uongozi uliopita," alisema Bumbuli.

Alisema pesa iliyolipwa ni Sh. milioni 52 kwa jumla, huku kati ya hizo, Sh. milioni 48 zikiwa ni zile ambazo Tambwe anadai na Sh. milioni 3.7 zikiwa ni gharama za mawakili.



# KAGERE, DUBE WAKABANA KOO UFUNGAJI BORA BARA

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba, wakikimbizana na watani zao, Yanga, kwenye kinyang'anyiro cha kuwania taji hilo, upande wa pili wa shilingi kuna mbio kali za kuwania Kiatu cha Dhahabu cha mfungaji bora wa ligi hiyo kati ya Meddie Kagere na Prince Dube.

**Simba ambayo inashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 55 baada ya kushuka dimbani mara 23, inafukuzia kuishusha Yanga kileleni ambayo inaizidi kwa pointi mbili, lakini ikiwa mbele michezo mitatu.**

Kwenye orodha ya wafungaji, straika wa Simba, Mnyarwanda Kagere anachuana vikali na mshambuliaji wa Azam FC, Mzibabwe Prince Dube kila mmoja akiwa na mabao 11 wakifukuziwa kwa karibu na Mtanzania John Bocco aliyecheka na nyavu mara 10 hadi sasa.

Watanzania wengine waliopo katika nafasi nzuri ya kutoa upinzani katika mbio hizo ni Danny Lyanga wa JKT Tanzania, Fully Maganga (Ruvu Shooting) na Meshack Abraham wa Gwambiana FC, kila mmoja akiwa na mabao nane mkononi mwake.

Hata hivyo, Kagere na Bocco pamoja na Abraham leo watakuwa na nafasi ya kuongeza idadi ya mabao endapo makocha wao watawapanga wakati Simba na Gwambina FC zitakaposhuka Uwanja wa Gwambina, Misungwi nje kidogo ya Jiji la Mwanza kwenye mwendelezo wa ligi hiyo.

Dube ambaye alikuwa na mabao 10 sawa na Bocco, juzi alirejea kwa kishindo na kumfikia Kagere, baada ya kucheka na nyavu wakati Azam ikilazimisha sare ya mabao 2-2 dhidi ya Dodoma Jiji FC, katika mechi iliyopigwa Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Hata hivyo, kasi ya mabao kwa Kagere ambaye msimu uliopita alitwaa Kiatu hicho kwa mara ya pili mfululizo, inaonekana kupungua msimu huu kutokana na kucheza kwa kupokezana na Bocco pamoja na Mkongomani Chris Mugalu mwenye mabao sita Simba.

Msimu uliopita, Kagere alimaliza akiwa na mabao 22 na endapo atatwaa Kiatu hicho atakuwa straika wa kwanza katika historia ya Ligi Kuu Bara kushinda tuzo hiyo mara tatu mfululizo.

Simba imebakiza mechi 11 kabla ya msimu kumalizika, wakati timu zingine zikiwa zimebakiza mechi nane, hivyo bado washambuliaji wake, Kagere na Bocco na hata Mugalu wana nafasi zaidi ya kubeba Kiatu hicho.

## MWINGINE TENA...



Kocha wa zamani wa viungo wa Raja Casablanca ya Morocco, Mmorocco Jawad Sabri (katikati), akiwa na viongozi wa Yanga baada ya kutambulishwa kujiunga na klabu hiyo jana, ambapo sasa atasaidiana na Watunisia, Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi na Msaidizi wake, Sghir Hammadi. **PICHA: YANGA**

# *Namungo yageuzia hesabu Ligi Kuu*

**Na Saada Akida**

BAADA ya kushindwa kufanya vizuri Kombe la Shirikisho barani Afrika, Kocha Mkuu wa Namungo FC, Hemed Morocco, amesema akili na nguvu zao sasa wanazielekeza kutafuta matokeo mazuri kwenye michezo yao iliyobaki ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Namungo FC, ambayo imetoka kupoteza mechi ya tano mfululizo kwenye michuano ya CAF huku ikiburuza mkia katika Kundi lake la D, inashuka dimbani leo (Jumamosi) kuwakaribisha Mbeya City, kwenye Uwanja wa Majaaliwa mkoani Lindi.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Morocco alisema walishindwa kufanya vizuri katika michuano hiyo, sasa wanalazimika kutuliza akili na nguvu zao kutafuta matokeo chanya kwenye Ligi Kuu ili kupata nafasi nyingine ya kushiriki michuano ya kimataifa msimu ujao.

Alisema kuna vitu wamejifunza katika michuano ya kimataifa licha ya kuendelea kupata matokeo mabaya katika michuano hiyo ila sasa wanarejea kwenye ligi ya nyumbani na hawana muda wa kupoteza katika kupambana kutafuta pointi kila mechi.

"Baada ya kumalizana na Raja Club Athletic ya Morocco na kukubali kichapo cha mabao 3-0, kwa matokeo hayo hayatufanyi kuwa wanyonge, sasa tunahitaji kuweka mikakati yetu imara kwenye ligi ya nyumbani ili tupate nafasi ya kushiriki kwa mara nyingine michuano ya kimataifa kwa msimu ujao," alisema Morocco.

Alisema ligi imekuwa na ushindani mkubwa hali inayowafanya kuhakikisha wanapambana kutafuta matokeo chanya ambayo yatawasaidia kuendelea kucheza Ligi Kuu na michuano ya kimataifa msimu ujao.

Namungo FC iko kwenye nafasi ya 11 ikiwa na pointi 31 zilizotokana na michezo 21 waliyocheza, wakati huu wakiwa na viporo vitano.

# Michezo

Jumamosi Aprili 24, 2021

Nipashe



Messi ajiwekea tena rekodi nyingine Ulaya UKURASA 22

HUNIPATI...



Mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi, akiambaa na mpira kulichungulia lango la Getafe wakati alipoifungia timu yake mabao mawili kwenye ushindi wa 5-2, huku beki Djene Dakonam, akimfukuzia kwenye mechi hiyo ya LaLiga iliyopigwa Uwanja wa Camp Nou juzi. **PICHA: MTANDAO**

## Kwasi achafua hewa, TFF, Simba wamkana

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Klabu ya Simba umeweka wazi kwamba hakuna taarifa rasmi waliopokea kutoka Shirikisho la Soka duniani (Fifa), kuhusu kufungiwa kusajili wachezaji wa kigeni msimu ujao kwa kipindi cha mwaka mmoja kutokana na madai ya kutomlipa aliyekuwa beki wa timu hiyo, Mghana Asante Kwasi.

Kwa mujibu wa barua ambayo inaelezwa waliandikiwa Simba kutoka Chama cha Soka cha Ghana (PFG), Februari 26, mwaka huu wakati huo ikiwa chini ya Ofisa Mtendaji Mkuu, Senzo Mbatha, kiliwaeleza kuwa wanapaswa kumlipa mchezaji huyo stahiki zake kiasi cha Dola za Marekani 4,000, baada ya kushinda rufaa yake, lakini hilo halikutekelezwa kwa wakati.

Hata hivyo, akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mwenyekiti wa Klabu ya Simba, Murtaza Mangungu, alisema hawana taarifa hizo na klabu hiyo haina muda wa kujibu kila jambo linalotoka kwenye mitandao.

Alisema chama cha kutetea wachezaji Ghana hakina mamlaka ya kuishtaki Simba kwa sababu mchezaji yeyote awe mzawa au wa kigeni wanakuwa wanachama wa nchi ambayo wanachezea ambapo kwa Tanzania ni SPUTANZA.

"Hizo taarifa hazina ukweli, hicho chama kinatakiwa kupeleka malalamiko ya mchezaji huyo shirikisho la nchi husika hapa kwetu (TFF) au SPUTANZA ambao ndio wenye mamlaka ya kutoa amri hiyo," alisema Mangungu.

Alipotafutwa Ofisa Habari wa TFF, Clifford Ndimbo, kujua endapo shirikisho hilo lina taarifa za Simba kufungiwa kusajili ama kutakiwa kumlipa Kwasi, alisema: "Hakuna taarifa yoyote au barua iliyofikia katika idara yangu.

"Suala lolote la Fifa au CAF ikitaka kuadhibu klabu ya nchini husika lazima taarifa zifike TFF, kwani ndio wenye kumiliki klabu za hapa nchini, kuhusu suala hilo la Simba hakuna taarifa au barua iliyofika kwenye idara yangu."

# Moshi mweupe Simba na FCC

**Na Mwandishi Wetu**

## ●●● Ni uwekezaji wa Bilionea Mo Dewji, sasa kimeeleweka baada ya waziri kusema...

MOSHI sasa mweupe! Ndivyo unavyoweza kusema kuhusu uwekezaji wa mfanyabiashara maarufu, Bilionea Mohamed "Mo" Dewji, katika Klabu ya Simba, baada ya kutatuliwa kwa vikwazo vilivyojitokeza.

**Wiki iliyopita, Bunge liliitaka serikali kuhakikisha inamaliza vikwazo vilivyojitokeza katika uwekezaji wa mfanyabiashara huyo, Spika wa Bunge, Job Ndugai, akinyooshea kidole vikwazo vinavyowakabili wawekezaji nchini.**

Katika mkutano wake na wanachama wa Shirikisho la Wenye Viwanda (CTI) jijini Dar es Salaam jana, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Geofrey Mwambe, alisema mazungumzo baina ya pande husika yamefanyika vizuri.

"Suala la uwekezaji ndani ya Klabu ya Simba, tulilipeleka FCC (Tume ya Ushindani). FCC wakalichukua kama suala la kisheria, ni kwa sababu Simba ilianzisha kampuni nyingi pale katikati. Kilichofanyika wakaziunganisha, ndipo FCC walipoona kama sheria imekiukwa kwenye uunganishaji wa hizo kampuni.

"Lakini huu ni uwekezaji, na sisi serikali tunahamasisha uwekezaji. Sasa tukaenda kuwaambia kwamba hili suala lisipelekwe kisheria, ni suala la kuzungumza.

"Kweli walianza kuzungumza na mazungumzo yamekwenda vizuri, kila kitu kitamalizika kwa mazungumzo, yataisha. Serikali imejipanga kwenye uwekezaji. Mwekezaji ukiwa na jambo linakutatiza, njoo tuzungumze," alisema.

Ijumaa ya wiki iliyopita, serikali ilijiarifu Bunge kuwa vikwazo vilivyoibuka katika uwekezaji wa Mo Dewji katika Klabu ya Simba vilitarajiwa kumalizika Jumatatu ya wiki hii, siku ambayo ilipangwa kuwa ya tatu na ya mwisho kwa FCC kukutana na pande zinazohusika.

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, ndiye aliyetoa kauli hiyo bungeni siku hiyo baada ya kutokea mjadala mkali kuhusu suala hilo.

Mjadala huo uliibuliwa na Mbunge wa Mlalo jijini Tanga, Rashid Shangazi (CCM), aliyeshika shilingi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, akiitaka serikali kumaliza ukiritimba kwenye uwekezaji nchini, akiutolea mfano uwekezaji wa Mo Dewji katika klabu hiyo kongwe nchini.

Spika Ndugai, aliyekuwa anaongoza kikao cha Bunge siku hiyo, alisema wanataka suala hilo limalizwe haraka, akisisitiza: "Haiwezekani klabu kubwa inayojiandaa kwa hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kukwamishwa kwa jambo dogo ambalo limechukua miaka mingi. Tunataka limalizwe haraka na wenzetu wa upande wa pili (Yanga) wajifunze."

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >